

Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.

Budget Documents

Budget Guidelines

2020

Mwongozo Wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti Ya Serikali Kwa Mwaka,2020- 2021


Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

<https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/729>

Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository

**MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA
BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2020/21**



SEHEMU YA KWANZA
SERA NA MFUMO WA BAJETI YA SERIKALI

YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA	iii
SERA NA MFUMO WA BAJETI YA SERIKALI	iii
ORODHA YA VIFUPISHO	vii
MUHTASARI.....	viii
SURA YA KWANZA.....	1
MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI.....	1
1.1 Utangulizi.....	1
1.2 Mwenendo wa Hali ya Uchumi.....	1
1.2.1 Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda.....	1
1.2.2 Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania.....	2
1.3 Mwelekeo wa Uchumi Jumla.....	6
1.3.1 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Dunia.....	6
1.3.2 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Tanzania.....	7
SURA YA PILI	9
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2018/19.....	9
2.1. Utangulizi.....	9
2.2. Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2018/19.....	9
2.2.1. Mapato ya Ndani	9
2.2.2. Matumizi	10
2.2.3. Misaada	10
2.2.4. Ugharamiaji wa Nakisi ya Bajeti.....	10
2.2.5. Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti	11
SURA YA TATU.....	20
MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/21.....	20
3.1. Utangulizi.....	20
3.2. Misingi ya Uchumi Jumla	20
3.3. Shabaha na Malengo ya Uchumi Jumla.....	20
3.4. Sera za Mapato na Makadirio katika Muda wa Kati	20
3.4.1. Sera za Mapato ya Ndani.....	20
3.4.2. Makadirio ya Mapato ya Ndani.....	21
3.5. Sera za Misaada na Makadirio kwa Muda wa Kati.....	23
3.6. Sera ya Kugharamia Nakisi ya Bajeti	23
3.6.1. Ukopaji kutoka Vyanzo vya Ndani.....	24
3.6.2. Ukopaji kutoka Vyanzo vya Nje.....	24

3.7.	Sera za Matumizi na Makadirio katika Muda wa Kati	25
3.7.1.	Sera za Matumizi.....	25
3.7.2.	Makadirio ya Matumizi	25
3.7.3.	Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kiuchumi	27
3.7.4.	Makadirio ya Matumizi Kisekta	28
3.8.	Vipaumbele katika Muda wa Kati.....	32
3.8.1.	Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda.....	32
3.8.2.	Maendeleo ya Watu.....	33
3.8.3.	Kuboresha Mazingira ya kufanya Biashara na Uwekezaji	33
3.8.4.	Kuongeza Ufanisi katika Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.....	34
SURA YA NNE.....		35
VIHATARISHI VYA KIBAJETI KWA MWAKA 2020/21		35
4.1.	Utangulizi.....	35
4.2.	Vihatarishi vya Uchumi Jumla.....	35
4.3.	Vihatarishi vya Bajeti.....	36
4.4.	Hatua za Kukabiliana na Vihatarishi.....	36
<i>Kiambatisho I</i>		38
MATUMIZI YALIYOAINISHWA KISEKTA KWA MAJUKUMU YA SERIKALI		38
<i>Kiambatisho II</i>		39
TAARIFA YA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA WIZARA/IDARA KWA MWAKA 2018/19		39
SEHEMU YA PILI.....		40
MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/21		40
SURA YA KWANZA.....		42
MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA		42
BAJETI KWA MWAKA 2020/21		42
1.1.	Uandaaji wa Mpango na Bajeti	42
1.2.	Maandalizi ya Bajeti ya Mishahara	42
1.2.1.	Kamati za Bajeti.....	42
1.2.2.	Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti.....	43
1.2.3.	Uchambuzi wa Mpango na Bajeti.....	43
1.2.4.	Majumuisho ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali	44

1.2.5.	Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep	44
1.3.	Mambo Mengine ya Kuzingatiwa katika Uandaaji wa Mpango na Bajeti.....	45
1.4.	Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa	52
1.4.1.	Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa	52
1.4.2.	Maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.....	53
1.5.	Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji.....	56
1.5.1.	Ufuatiliaji na Tathmini	56
1.5.2.	Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji	57
SURA YA PILI		58
MUUNDO WA UWASILISHAJI NA UTOAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/21		58
2.1.	Utangulizi.....	58
2.2.	Maandalizi ya Mpango na Bajeti	58
2.3.	Utekelezaji wa Bajeti.....	59
2.4.	Taarifa za Utekelezaji	59

ORODHA YA VIFUPISHO

AIDS	Acquired Immune Deficiency Syndrome
ATCL	Air Tanzania Company Limited
BOT	Bank of Tanzania
CBMS	Centralized Budget and Management System
CDR	Council Development Reporting
CFR	Council Financial Reporting
DCF	Development Cooperation Framework
DPs	Development Partners
EAC	East African Community
EU	European Union
FFARS	Facility Financial Accounting and Reporting System
FYDP	Five Year Development Plan
GePG	Government electronic Payment Gateway
GBS	General Budget Support
GFS	Government Finance Statistics
HIV	Human Immunodeficiency Virus
ICT	Information Communication Technology
IFMS	Integrated Financial Management Systems
JNIA	Julius Nyerere International Airport
KIA	Kilimanjaro International Airport
LGAs	Local Government Authorities
M3	Extended Broad Money Supply
MDAs	Ministries, Independent Departments and Agencies
MTEF	Medium Term Expenditure Framework
MTSPBM	Medium Term Strategic Plan and Budget Manual
MW	Megawatts
NFRA	National Food Reserve Agency
NHIF	National Health Insurance Fund
OC	Other Charges
PE	Personnel Emoluments
PIM-OM	Public Investment Management - Operational Manual
PlanRep	Planning and Reporting Database
PPP	Public Private Partnership
REA	Rural Energy Agency
SADC	Southern Africa Development Community
SIDO	Small Industry Development Organisation
SME	Small and Medium Enterprise
TEA	Tanzania Education Authority
TMX	Tanzania Mercantile Exchange
TRA	Tanzania Revenue Authority
VAT	Value Added Tax

MUHTASARI

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti wa Mwaka 2020/21 umeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439. Mwongozo huu unatoa maelekezo ya jumla na mahsusi ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wakati wa uandaaji na utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2020/21 ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2025.

Mwongozo wa Mpango na Bajeti unawaelekeza Maafisa Masuuli kuandaa mpango na bajeti kwa kuzingatia: Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21; Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015; Maelekezo ya Serikali yaliyoainishwa na Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi rasmi wa Bunge la 11 mwezi Novemba 2015; Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na Kanuni zake; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu; Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada Sura, 134; Malengo ya Maendeleo Endelevu; Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo; na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Serikali imeyaridhia.

Mwongozo huu umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya Kwanza inaelezea Sera na Mfumo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/21. Sehemu hii imegawanyika katika Sura nne ambazo ni (i) Mapitio ya Mwenendo na Mwelekeo wa Hali ya Uchumi, ambapo imeeleza mwenendo wa uchumi wa dunia, ukanda wa Jumuiya za SADC na EAC na uchumi wa Tanzania; (ii) Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2018/19; (iii) Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2020/21, ambapo imeainisha maeneo ya sera za mapato na matumizi, makadirio ya mapato na matumizi na vipaumbele vya Serikali kwa mwaka 2020/21; na (iv) Vihatarishi vya Kibajeti kwa Mwaka 2020/21 na hatua za kukabiliana navyo. Sehemu ya Pili inatoa maelekezo ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wote katika uandaaji, uwasilishaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2020/21.

Mwaka 2018, uchumi wa Tanzania uliimarika, ambapo Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2017 kutokana na kuongezeka kwa uwekezaji hususan katika miundombinu ya ujenzi wa barabara, reli na viwanja vya ndege; kutengemaa kwa upatikanaji wa nishati ya umeme; kuimarika kwa huduma za usafirishaji; na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya sekta ya kilimo kulikotokana na hali nzuri ya hewa. Mwaka 2019, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.0 na kuongezeka kwa wastani wa asilimia 7.1 katika muda wa kati. Ukuaji huu utachochewa na: uwekezaji katika miradi ya miundombinu; utekelezaji wa

Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara; na azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda kupitia mageuzi ya sekta ya kilimo.

Katika mwaka 2018/19, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 18,529.6 ambapo mapato yaliyokusanywa na TRA yalikuwa shilingi bilioni 15,511.3, mapato yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 2,356.9 na mapato ya Halmashauri yalikuwa shilingi bilioni 661.4. Kadhalika, Serikali ilikopa shilingi bilioni 3,950.7 katika masoko ya ndani ambapo shilingi bilioni 3,319 zilikuwa ni kwa ajili ya kulipia deni la ndani na shilingi bilioni 631.7 zilikuwa kwa ajili ya kugharamia nakisi ya bajeti. Kwa upande mwingine, Serikali ilitoa ridhaa ya matumizi ya shilingi bilioni 27,049.2 ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 19,099.9 na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 7,949.3.

Katika muda wa kati, mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Halmashauri yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 27,759.3 kutoka shilingi bilioni 23,045.3 mwaka 2019/20. Mapato ya kodi yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 23,419.3 kutoka shilingi bilioni 18,955.2 mwaka 2019/20. Matumizi ya Serikali yanakadiriwa kukua hadi shilingi bilioni 37,684.3 mwaka 2022/23 kutoka shilingi bilioni 33,105.4 mwaka 2019/20. Aidha, matumizi ya kawaida na maendeleo yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 23,741.6 na shilingi bilioni 13,942.7 mwaka 2022/23 kutoka shilingi bilioni 20,856.8 na shilingi bilioni 12,248.6 mwaka 2019/20 mtawalia.

Katika mwaka 2020/21, Serikali itasimamia vipaumbele vifuatavyo: Kuimarisha na kusimamia mifumo ya ukusanyaji wa mapato; kuboresha na kupanua huduma za elimu, afya na maji; kuendelea kuimarisha sekta ya kilimo kwa kuboresha upatikanaji wa mbegu na pembejeo za kilimo pamoja na kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji, maghala na masoko; kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji; na kuimarisha mindombinu ya nishati, barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege, madaraja na vivuko. Aidha, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ikijumuisha mradi wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere; ujenzi wa reli ya kati ya "Standard Gauge" na kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL). Vile vile, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele katika kudumisha amani, ulinzi na usalama; kuimarisha mifumo na taasisi za utoaji haki na kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa huduma za kisheria; na kuendeleza utawala bora na demokrasia ikiwemo shughuli za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Malengo ya mpango na bajeti yanalenga kuimarisha makusanyo kwa kutekeleza hatua za kiutawala zikiwemo kuboresha mazingira ya kufanya biashara na

uwekezaji, kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi, usimamizi wa sheria za kodi, kupunguza upotevu wa mapato; na kuwianisha na kupunguza tozo na ada mbalimbali zinazotozwa na Wakala za Serikali na Mamlaka za Udhibiti. Aidha, sera za matumizi zitalenga kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma, kuelekeza fedha kwenye miradi ya kimkakati inayochochea ukuaji wa uchumi, kudhibiti ulimbikizaji wa madeni, ulipaji wa deni la Serikali, kugharimia Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 na kuhakikisha nakisi ya bajeti haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa.

Katika kufanikisha malengo hayo, Mwongozo umeainisha masuala ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na utoaji wa taarifa. Baadhi ya maelekezo hayo ni pamoja na: kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti na kubuni mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye Mafungu; kuandaa mpango na bajeti kwa kuzingatia muundo wa Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi; kuzingatia viwango vya ukomo wa bajeti vitakavyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango; kujumuisha gharama za miradi inayoendelea katika bajeti kabla ya kuanzisha miradi mipya; kufanya ukadiriaji sahihi wa matumizi yasiyoepukika hususan stahili za kisheria za kiutumishi, gharama za pango, umeme, simu, maji, ulinzi na usafi; kutenga fedha za kulipia madeni yaliyohakikiwa; kuandaa ikama na makadirio ya bajeti ya mishahara kwa kuzingatia Waraka wa Katibu Mkuu UTUMISHI; kuandaa mpango kazi na mpango wa mahitaji ya fedha kwa wakati; kuhakikisha Kamati za Bajeti za Mafungu zinafanya kazi kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 18(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake; na kuandaa taarifa za utekelezaji kwa kuzingatia muundo ulioainishwa katika Sura ya Pili ya Mwongozo.

SURA YA KWANZA

MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA HALI YA UCHUMI

1.1 Utangulizi

1. Sura hii inaelezea mapitio pamoja na mwelekeo wa hali ya uchumi. Katika kipindi hicho, bajeti ya Serikali ililenga katika kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 - 2020/21 na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015 ili kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Vipaumbele hivyo ni: Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda; Kufungamanisha Maendeleo ya Viwanda na Maendeleo ya Watu; Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji; na Kuimarisha Usimamizi wa Utekezaji wa Mpango. Katika kipindi hicho, mwenendo wa hali ya uchumi ulitengemaa kutokana na utekezaji wa sera mbalimbali.

1.2 Mwenendo wa Hali ya Uchumi

1.2.1 Hali ya Uchumi wa Dunia na Kikanda

(a) Ukuaji wa Uchumi

2. Katika mwaka 2018, uchumi wa dunia ulikua kwa asilimia 3.6 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.8 mwaka 2017 na unakadiriwa kukua kwa asilimia 3.5 mwaka 2019. Kasi ndogo ya ukuaji ilichangiwa na mgogoro wa kibiashara baina ya China na Marekani, kuendelea kutotabirika kwa hatima ya Uingereza kujitoka katika Jumuiya ya Umoja wa Ulaya, kudorora kwa masoko ya fedha ya Argentina na Uturuki pamoja na machafuko ya kisiasa katika nchi za Mashariki ya Kati. Kuendelea kwa mgogoro baina ya China na Marekani inaweza kuathiri kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi mbalimbali Duniani ikiwemo Tanzania.

3. Katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), ukuaji wa uchumi umeendelea kuimarika kidogo kutoka wastani wa asilimia 3.1 mwaka 2017 hadi asilimia 3.2 mwaka 2018. Ongezeko hili lilichangiwa na kuimarika kwa uchumi wa nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Botswana. Aidha, Tanzania imeendelea kuongoza kwa kasi ya ukuaji wa uchumi kwa wastani wa asilimia 6.9 kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo. Hata hivyo, Angola na Namibia zimekuwa na ukuaji hasi wa wastani wa asilimia 1.7 na asilimia 0.1 mtawalia. Hali hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kudorora kwa sekta ya mafuta kulikotokana na uwekezaji mdogo na ufikiaji wa ukomo wa visima vya kuzalisha mafuta kwa nchi ya Angola na matokeo yasiyoridhisha katika sekta za uzalishaji kutokana na ukame katika nchi ya Namibia.

4. Mwenendo wa uchumi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki umeendelea kuimarika. Uchumi wa nchi hizi ulikua kwa wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2018 kutoka asilimia 4.4 mwaka 2017. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na shughuli za kilimo, ujenzi, utoaji huduma, usafirishaji na uzalishaji viwandani.

(b) Mfumuko wa Bei

5. Mfumuko wa bei wa dunia kwa mwaka 2018 uliongezeka na kufikia asilimia 3.6 kutoka asilimia 3.2 mwaka 2017 kutokana na kuongezeka kwa bei za mafuta hususan katika kipindi cha miezi tisa ya mwanzo ya mwaka 2018. Hata hivyo, mfumuko wa bei kwa nchi nyingi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ulishuka hadi asilimia 8.5 mwaka 2018 kutoka asilimia 11.0 mwaka 2017 kutokana na kupungua kwa bei za vyakula kulikochangiwa na hali nzuri ya hewa.

6. Mfumuko wa bei katika nchi nyingi za ukanda wa SADC ulipungua hadi asilimia 8.2 mwaka 2018 ukilinganishwa na asilimia 9.9 mwaka 2017. Mwenendo huo ulitokana na kupungua kwa bei za vyakula kulikochangiwa na hali nzuri ya hewa na utulivu wa viwango vya ubadilishaji fedha.

7. Katika mwaka unaoishia mwezi Juni 2019, wastani wa mfumuko wa bei katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulipungua na kufikia asilimia 1.7 kutoka wastani wa asilimia 4.5 mwaka unaoishia mwezi Juni 2018. Hii ni kutokana na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika nchi hizo. Kiwango hiki kipo ndani ya wigo wa mfumuko wa bei uliokubalika kikanda usiozidi asilimia 8.0.

1.2.2 Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania

(a) Ukuaji wa Pato la Taifa

8. Katika kipindi cha muongo mmoja, uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika ambapo Pato la Taifa kwa bei za kizio cha mwaka 2015 limekua kwa wastani wa asilimia 6.4 kwa mwaka. Ukuaji wa Pato la Taifa ulikuwa asilimia 7.0 mwaka 2018 ukilinganishwa na asilimia 6.8 mwaka 2017. Aidha, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019 (Januari – Juni), Pato la Taifa kwa mwaka wa kizio wa 2015 lilikua kwa asilimia 6.9 ikilinganishwa na asilimia 6.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Ukuaji huu ulichochea zaidi na kuongezeka kwa uwekezaji hususan katika miundombinu kama vile ujenzi wa barabara, reli na viwanja vya ndege; kutengemaa kwa upatikanaji wa nishati ya umeme; kuimarika kwa huduma za usafirishaji; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini hususan dhahabu na makaa ya mawe; na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao ya sekta ya kilimo kulikotokana na hali nzuri ya hewa. Sekta zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji kwa kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2019 ni pamoja na ujenzi (asilimia 16.5), uchimbaji

madini na mawe (asilimia 13.7), habari na mawasiliano (asilimia 10.7), maji (asilimia 9.1) na usafirishaji na uhifadhi wa mizigo (asilimia 9.0).

(b) Mfumuko wa bei

9. Mfumuko wa bei uliendelea kubakia ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0 katika mwaka ulioishia mwezi Juni 2019. Katika kipindi hicho, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.2 ukilinganishwa na asilimia 4.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Hali hii ilichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji na upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na nchi jirani na utekelezaji thabiti wa sera za fedha na bajeti. Mfumuko wa bei ulifikia asilimia 3.4 Septemba 2019 kama ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018.

10. Mfumuko wa bei za vyakula ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 1.4 katika mwaka ulioishia mwezi Juni 2019 ukilinganishwa na asilimia 6.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Aidha, katika kipindi hicho mfumuko wa bei usiojumuisa bei za vyakula na nishati ulifikia wastani wa asilimia 2.8 ukilinganishwa na asilimia 1.6.

(c) Mwenendo wa Ujazi wa Fedha na Karadha

11. Katika kipindi cha mwaka 2018/19, Benki Kuu iliendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi¹ kwenye uchumi katika mazingira ya utulivu wa mfumuko wa bei. Utekelezaji wa sera hiyo ulilenga kuziwezesha benki na taasisi za fedha kuongeza kasi ya utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kukuza shughuli mbalimbali za uchumi. Kufuatia utekelezaji huo, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua na kufikia asilimia 8.5 Agosti 2019 ikilinganishwa na asilimia 6.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Maendeleo haya yametokana na kukua kwa mikopo ya ndani. Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa asilimia 8.2 Agosti 2019 ikilinganishwa na asilimia 5.2 Agosti 2018.

12. Ukuaji wa mikopo ulijidhihirisha zaidi katika shughuli kuu za kiuchumi kama vile kilimo (asilimia 40.6), uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 28.4), shughuli binafsi (asilimia 17.4) na viwanda vya uzalishaji (asilimia 14.5). Wanufaika wakuu wa mikopo kutoka benki ni wale waliokuwa wakijihusisha na shughuli binafsi na biashara ambapo mikopo binafsi ilikuwa asilimia 29.2 na mikopo ya biashara ilikuwa asilimia 18.0 Agosti 2019.

¹ Benki Kuu ilipunguza riba ya mikopo kwa benki (*discount rate*) kutoka asilimia 9.0 hadi asilimia 7.0 mwezi Agosti 2018, pamoja na kuendelea kutumia zana za sera ya fedha kuongeza ukwasi ikiwamo: kununua fedha za kigeni, na kuendelea kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki (*Lombard, intraday loans and discount window*).

(d) Mwenendo wa Viwango vya Riba

13. Kwa ujumla, riba za mikopo zilipungua kufikia wastani wa asilimia 16.77 Agosti 2019 kutoka asilimia 17.09 Agosti 2018. Vile vile, riba za mikopo za mwaka mmoja zilipungua kufikia asilimia 16.34 Agosti 2019 kutoka asilimia 18.19 Agosti 2018. Aidha, riba za amana kwa ujumla zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 7.01 Agosti 2019 kutoka asilimia 7.63 Agosti 2018. Hata hivyo, riba za amana za miezi 12 ziliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 8.86 Agosti 2019 kutoka asilimia 7.75 Agosti 2018. Kufuatia mwenendo huo, tofauti ya viwango vya riba ya kukopa na ya amana ya mwaka mmoja ilipungua na kufikia asilimia 7.48 kutoka asilimia 10.44 katika kipindi hicho.

(e) Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji Fedha

14. Thamani ya Shilingi ya Tanzania imeendelea kuwa tulivu dhidi ya dola ya Marekani kufuatia utekelezaji wa sera ya fedha na usimamizi thabiti wa bajeti ya Serikali. Kwa mwaka 2018/19, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,293.1, ikilinganishwa na shilingi 2,254.4 katika mwaka 2017/18, ikiwa ni sawa na ongezeko la gharama ya kubadilisha fedha la asilimia 1.7 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 1.85 mwaka 2017/18.

(f) Mwenendo wa Sekta ya Benki

15. Sekta ya benki imeendelea kuwa imara, salama na yenye faida, ikiwa na mtaji na ukwasi wa kutosha zaidi ya kiwango kinachotakiwa kisheria. Kwa mwezi Agosti 2019, kumekuwa na ongezeko la mapato na faida kutokana na uwekezaji katika rasilimali na mtaji ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2018. Faida kutokana na uwekezaji wa rasilimali iliongezeka kutoka asilimia 6.88 Agosti 2018 hadi 8.16 Agosti 2019 na faida kutokana na uwekezaji wa mtaji iliongezeka kutoka asilimia 1.68 Agosti 2018 hadi 1.89 Agosti 2019.

16. Thamani ya rasilimali za benki iliimarika kama inavyojidhihirisha katika mikopo chechefu ambayo ilipungua kufikia asilimia 10.7 kwa mwaka ulioishia Juni 2019 kutoka asilimia 11.3 Juni 2018. Mwenendo huu ulichochea na hatua² mbalimbali zilizochukuliwa na Benki Kuu ikiwa ni pamoja na kuzielekeza benki na taasisi za fedha kutekeleza mikakati ya kupunguza mikopo chechefu na kutoa taarifa kila robo mwaka (Jedwali 1.1).

² Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuzitaka benki na taasisi za fedha; kuboresha usimamizi katika utoaji mikopo; kuwasilisha mpango kazi wa kupunguza uwiano wa mikopo chechefu kwa benki zilizokuwa na uwiano mkubwa; na kuhamasisha matumizi ya Kanzidata ya Taarifa za Wakopaji (*credit reference system*) kabla va utoaji wa mikopo

Jedwali 1.1: Mwenendo wa Viashiria vya sekta ya Benki (Asilimia)

Kiashiria	Ukomo	Jun-18	Des-18	Mar-19	Jun-19
Utosholevu wa mtaji					
Uwiano wa mtaji wa msingi kwa rasilimali za benki	Kiwango cha chini 10	18.21	16.20	15.93	16.23
Ukwasi					
Uwiano wa rasilimali zenye ukwasi kwa amana zinazoweza kuhitajika muda mfupi	Kiwango cha chini 20	37.60	35.22	34.33	34.81
Uwiano wa mikopo kwa amana za wateja		83.94	85.07	88.65	84.51
Mapato na faida					
Faida kutokana na uwekezaji wa rasilimali		1.60	1.04	1.73	1.96
Faida kutokana na uwekezaji wa mtaji		6.65	2.88	7.39	8.80
Ubora wa rasilimali					
Uwiano wa mikopo chechefu kwa mikopo yote		11.27	10.51	10.87	10.70

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

(g) Deni la Serikali

17. Deni la Serikali lilifikia shilingi bilioni 52,303.04 Agosti 2019 kutoka shilingi bilioni 49,283.44 Agosti 2018. Kati ya Deni hilo, shilingi bilioni 38,227.86 ni deni la nje na shilingi bilioni 14,075.18 ni deni la ndani. Hali hiyo ilitokana na mikopo mipya ya hati fungani na dhamana za Serikali pamoja na mikopo kutoka nje kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hivyo, deni la Serikali limeendelea kuwa himilivu.

(h) Mwenendo wa Sekta ya Nje

18. Urari wa malipo nje ya nchi ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,059.6 Juni 2019 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 627.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2018. Hali hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa nakisi ya urari wa malipo ya kawaida unaojumuisha biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali nje ya nchi. Urari wa malipo ya kawaida ulionesha nakisi ya dola za Marekani milioni 2,257.3 Juni 2019 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,771.7 katika kipindi kama hicho mwaka uliotangulia kutokana na kuongezeka kwa thamani ya uagizaji wa bidhaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kushuka kwa mauzo ya bidhaa nje (Jedwali 1.2). Akiba ya fedha za kigeni (bila kujumuisha bidhaa na huduma ambazo zinalipiwa na fedha za uwekezaji wa moja kwa moja) ilikuwa dola za Marekani milioni 5,200.1 Agosti 2019 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,500.5 Agosti 2018, ambayo inatosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 6.0. Hali hii ilitokana na mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na malipo ya madeni ya nje.

Jedwali Na. 1.2: Urari wa Malipo ya Kawaida*Dola milioni*

	2017/18	2018/19 ^P	Badiliko %
Bidhaa	-2,974.2	-3,853.4	29.6
Mauzo Nje	4,691.9	4,493.6	-4.2
Uagizaji Nje	7,666.1	8,347.0	8.9
Huduma	1,720.7	2,035.6	18.3
Mapato	3,896.6	4,068.0	4.4
Malipo	2,175.9	2,032.4	-6.6
Bidhaa na Huduma	-1,253.5	-1,817.8	45.0
Mauzo ya bidhaa na huduma	8,588.5	8,561.6	-0.3
Uagizaji bidhaa na huduma	9,842.0	10,379.4	5.5
Mapato ya Vitega uchumi	-952.7	-820.1	-13.9
Mapato	138.6	191.2	38.0
Malipo	1,091.3	1,011.3	-7.3
Uhamisho wa Mali	434.5	380.6	-12.4
Zilizolingia	521.1	440.2	-15.5
Kwa Serikali Kuu	155.3	68.2	-56.1
Zilizotoka	86.6	59.6	-31.2
Urari wa Malipo ya Kawaida	-1,771.7	-2,257.3	27.4

*Chanzo: Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania***1.3 Mwelekeo wa Uchumi Jumla****1.3.1 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Dunia**

19. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia ya Shirika la Fedha la Kimataifa, toleo la Julai, 2019, uchumi wa dunia unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.2 mwaka 2019 kutoka asilimia 3.6 mwaka 2018 na kuongezeka kufikia asilimia 3.5 mwaka 2020 (**Jedwali 1.3**). Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi mwaka 2019 kunatarajiwa kuchangiwa na: athari za mgogoro wa kibiashara baina ya China na Marekani; matokeo yasiyoridhisha na yasiyoakisi juhudi zinazofanywa na Marekani kupitia vichocheo vya kifedha kukuza uchumi; na uwekezaji hafifu wa sekta binafsi kwa uchumi wa nchi zilizoendelea na zinazoibukia.

20. Kiwango cha ukuaji wa uchumi katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara kinatarajiwa kuongezeka na kufikia asilimia 3.6 mwaka 2020 kutoka matarajio ya ukuaji wa wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2019. Ukuaji huu utachangiwa kwa kiasi kikubwa na ukuaji wa uchumi wa nchi zisizo na rasilimali asilia na ongezeko la

uwekezaji katika miundombinu kwa nchi husika.

Jedwali Na. 1.3: Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Maoteo (Asilimia)

	Halisi		Maoteo	
	2017	2018	2019	2020
Dunia	3.8	3.6	3.2	3.5
Nchi Zilizoeendelea	2.4	2.2	1.9	1.7
Nchi Zinazoendelea na Kuibuka	4.8	4.5	4.1	4.7
China	6.8	6.6	6.2	6.0
India	7.2	6.8	7.0	7.2
Nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara	2.9	3.1	3.4	3.6

Chanzo: Shirika la Fedha la Kimataifa, Julai, 2019

1.3.2 Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Tanzania

(a) Ukuaji wa Pato la Taifa

21. Uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.0 kwa mwaka 2019 na kufikia wastani wa asilimia 7.1 katika muda wa kati. Mwenendo huu unachochewa na uendelezaji wa uwekezaji katika miradi ya miundombinu, utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhhibiti wa Biashara pamoja na azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda kupitia mageuzi ya sekta ya kilimo.

(b) Mfumuko wa Bei

22. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa ndani ya wigo uliokubalika kikanda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki usiozidi asilimia 8.0 katika kipindi cha mwaka unaoishia Juni 2020. Katika muda wa kati, mfumuko wa bei unatarajiwa kuwa na kiwango kisichozidi asilimia 5.0 kutokana na: kuimarika kwa uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme kwa bei nafuu; kutengama kwa bei ya mafuta katika soko la dunia; sera madhubuti za bajeti; na kuimarika kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo kutokana na hali nzuri ya hewa nchini na ukanda wa Afrika Mashariki.

(c) Mwelekeo wa Sera ya Fedha

23. Katika mwaka 2019/20, Benki Kuu inakusudia kutekeleza Sera ya Fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi ili kuchochea ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi pamoja na shughuli za uchumi. Kufuatia utekelezaji wa sera hii, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) unatarajiwa kukua na kufikia asilimia 10.0 Juni 2020. Katika kipindi hicho, mikopo kwa sekta binafsi inatarajiwa kukua na kufikia asilimia 13.5 kutoka asilimia 7.6 Juni 2019. Mwelekeo wa sera ya fedha uko sanjari na malengo ya mfumuko wa bei unaotarajiwa kuwa ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 5.0. Aidha, sera ya fedha inalenga kuwa na akiba ya fedha za

kigeni inayokidhi kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

24. Katika mwaka 2020/21, Benki Kuu itaendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuweka mazingira tulivu ya riba katika masoko ya fedha na mfumuko wa bei wa tarakimu moja. Utekelezaji wa sera ya fedha chini ya mfumo mpya unaotumia riba ya Benki Kuu utawezesha kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa sera ya fedha katika kufikia malengo ya kudumisha utulivu wa mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi. Vile vile, Benki Kuu itaendelea kusimamia akiba ya fedha bila kuathiri mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

(d) Sekta ya Nje

25. Katika mwaka 2020/21, urari wa malipo ya kawaida unatarajiwa kuongezeka kutokana na uagizaji wa bidhaa za mtaji kwa ajili ya ujenzi wa miradi mikubwa ya kielelezo. Mauzo ya bidhaa nje yanatarajiwa kukua kutokana na mauzo ya madini kufuatia kuanzishwa kwa minada ya madini nchini.

SURA YA PILI

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2018/19

2.1. Utangulizi

26. Sura hii inaeleza mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/19 kama ilivyobainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21, Ilani ya CCM ya mwaka 2015, Maelekezo ya Serikali yaliyoainishwa na Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi rasmi wa Bunge la 11 Novemba 2015; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030. Lengo la mapitio ni kutathmini mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji ili kuboresha maandalizi ya mpango na bajeti kwa mwaka 2020/21. Mapitio yamefanywa katika baadhi ya miradi ya kielelezo, kimkakati na maeneo mengine ya kipaumbele. Tathmini hii imefanyika kwa kulinganisha malengo yaliyowekwa, mapato na matumizi halisi pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho.

2.2. Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2018/19

27. Mwaka 2018/19, Serikali ilitekeleza sera mbalimbali za mapato ya ndani zilizolenga kupanua wigo wa kodi, kuimarisha usimamizi wa vyanzo vilivyopo hususan kuhimiza matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato pamoja na hatua nyingine za kiutawala. Vile vile, utekelezaji wa mpango na bajeti ulizingatia Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo Tanzania pamoja na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134. Kwa upande mwingine, sera za matumizi zililenga kuwianisha mapato na vipaumbele vya matumizi na kuimarisha usimamizi wa fedha za umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439.

2.2.1. Mapato ya Ndani

28. Katika mwaka 2018/19, mapato ya ndani yalifikia shilingi bilioni 18,529.6, sawa na asilimia 88.7 ya lengo la shilingi bilioni 20,894.6. Kati ya kiasi hicho, mapato yaliyokusanywa na TRA yalikuwa shilingi bilioni 15,511.3 sawa na asilimia 86.2 ya malengo ya shilingi bilioni 18,000.2, mapato yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 2,356.9 ikiwa ni asilimia 109.2 ya lengo la shilingi bilioni 2,158.8 na mapato ya Halmashauri yalikuwa shilingi bilioni 661.4 sawa na asilimia 89.9 ya lengo la shilingi bilioni 735.6.

29. Kutofikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato ya kodi, kumetokana na sababu mbalimbali zikiwemo: changamoto ya uwekaji tozo katika sekta isiyo rasmi; upotevu wa mapato uliosababishwa na shughuli za magendo hasa kupitia bandari bubu katika ukanda wa bahari ya Hindi na njia zisizo rasmi mipakani; na ukwepaji kodi.

2.2.2. Matumizi

30. Katika mwaka 2018/19, Serikali ilitoa ridhaa ya matumizi ya shilingi bilioni 27,049.2, sawa na asilimia 83.3 ya makadirio ya shilingi bilioni 32,475.9. Kati ya kiasi cha shilingi bilioni 27,049.2 kilichotolewa, matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 19,099.9 sawa na asilimia 92.5 ya makadirio ya shilingi bilioni 20,642.6 na matumizi ya maendeleo yalikuwa shilingi bilioni 7,949.3 sawa na asilimia 67.2 ya makadirio ya shilingi bilioni 11,833.4.

(a) Matumizi ya Kawaida

31. Matumizi ya kawaida yalijumuisha: Mishahara shilingi bilioni 6,659.6 sawa na asilimia 89.9 ya makadirio ya shilingi bilioni 7,409.9; deni la Serikali shilingi bilioni 7,701.7, sawa na asilimia 92.0 ya makadirio ya shilingi bilioni 8,372.9; na matumizi mengineyo shilingi bilioni 4,738.6, sawa na asilimia 97.5 ya makadirio.

(b) Matumizi ya Maendeleo

32. Matumizi ya Maendeleo kwa mwaka 2018/19 yalikuwa shilingi bilioni 7,949.3 sawa na asilimia 67.2 ya makadirio ya shilingi bilioni 11,833.4. Kati ya kiasi kilichotumika, shilingi bilioni 6,496.2 zilitokana na fedha za ndani na shilingi bilioni 1,453.1 ni fedha za nje. Aidha, katika kipindi cha mapitio Serikali ilitumia shilingi bilioni 7,701.7 kwa ajili ya kulipa deni lililoiva la fedha zilizokopwa kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

2.2.3. Misaada

33. Misaada iliyopokelewa kwa mwaka 2018/19 ni shilingi bilioni 461.2, sawa na asilimia 43.0 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,081.4. Kati ya misaada hiyo, fedha za Mifuko ya Pamoja ya Kisekta ni shilingi bilioni 175.9 ikiwa ni asilimia 90.8 zaidi ya lengo la shilingi bilioni 92.2. Fedha za misaada ya miradi ya maendeleo zilikuwa shilingi bilioni 285.3, sawa na asilimia 38.0 ya makadirio ya shilingi bilioni 752.9.

2.2.4. Ugharamiaji wa Nakisi ya Bajeti

(a) Mikopo Nafuu

34. Mikopo nafuu iliyopokelewa mwaka 2018/19 ilikuwa shilingi bilioni 1,622.2 ikiwa ni asilimia 2.0 zaidi ya makadirio ya shilingi bilioni 1,595.2. Kati ya kiasi hicho, fedha za mikopo ya kibajeti ni shilingi bilioni 125.4 sawa na asilimia 41.0 ya makadirio ya shilingi bilioni 309.5, Mifuko ya Pamoja ya Kisekta shilingi bilioni 44.3 kati ya makadirio ya shilingi bilioni 33.7, sawa na asilimia 131.5 ya lengo na fedha za miradi ya maendeleo shilingi bilioni 1,452.5 sawa na asilimia 116.0 ya makadirio ya shilingi bilioni 1,252.0.

(b) Mikopo yenye Masharti ya Kibiashara

35. Katika mwaka 2018/19, Serikali ilikopa shilingi bilioni 1,144.8 kutoka vyanzo vya nje ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 3,111.1. Kutofikiwa kwa lengo la fedha za mikopo yenye masharti ya kibiashara kulitokana na masharti magumu ya taasisi za fedha duniani, kuimarika kwa dola ya Marekani na kuongezeka kwa riba. Aidha, Serikali ilikopa shilingi bilioni 3,950.7 kutoka masoko ya ndani sawa na asilimia 68.2 ya makadirio ya shilingi bilioni 5,793.7. Kati ya mikopo hiyo, shilingi bilioni 3,319.0 zilikuwa ni kwa ajili ya kulipia deni la ndani na shilingi bilioni 631.7 zilikuwa kwa ajili ya kugharamia nakisi ya bajeti.

2.2.5. Mafanikio ya Utekelezaji wa Bajeti

36. Sehemu hii inaelezea mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Mafanikio hayo ni pamoja na:

37. **Ulupaji wa Deni la Serikali:** katika kipindi cha 2016/17 hadi Septemba 2019, Serikali imefanikiwa kulipa jumla ya shilingi bilioni 24,499.2 kwa ajili ya deni lililoiva la fedha zilizokopwa kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

38. **Ulupaji wa Mishahara:** mishahara ya watumishi wa Serikali yenye jumla ya shilingi bilioni 22,169.9 ililipwa kwa wakati katika kipindi cha mwaka 2016/17 hadi Septemba 2019.

39. **Ukusanyaji wa Mapato:** kuongezeka kwa mapato ya kodi kutoka wastani wa shilingi bilioni 800 kwa mwezi katika mwaka 2016/17 kufikia wastani wa shilingi bilioni 1,292.6 kwa mwezi katika mwaka 2018/19 kutokana na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tan● ikiwemo kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato, kurahisisha ulupaji wa kodi na kuongeza mwitikio wa ulupaji kodi kwa hiari. Juhudi hizo zimeendelea kuleta mafanikio ambapo mapato ya kodi kwa mwezi Septemba 2019 yamefikia shilingi bilioni 1,785.0.

40. **Ujenzi wa Reli ya Kati ya Standard Gauge:** Katika mwaka 2018/19, Serikali iliendelea na ujenzi wa reli ya kati ya *Standard Gauge* ambapo kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro umefikia asilimia 63.0 na shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kutandika reli, ujenzi wa madaraja na makalavati, uwekaji wa nguzo za umeme pamoja na ujenzi wa stesheni za Dar es Salaam, Pugu na Soga. Vile vile, utekelezaji wa ujenzi kwa kipande cha Morogoro - Makutupora umefikia asilimia 16.0. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kukamilika kwa usanifu wa kina; ujenzi wa barabara ya kuhudumia mradi; usanifu wa stesheni na majengo mengine pamoja na uchorongaji wa mahandaki mawili ya njia ya reli eneo la Kilosa. Jumla ya shilingi trilioni 2.52 zimetumika katika kugharamia mradi huu ambapo kwa mwaka 2018/19 zilitolewa shilingi bilioni 455.6.

41. **Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere:** Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi huu unaotarajiwa kugharimu shilingi bilioni 6,558.6 na kuongeza kiwango cha umeme kwa Megawati 2,115 kwenye gridi ya Taifa ifikapo mwaka 2022. Katika mwaka 2018/19, shilingi bilioni 1,047.0 zilitumika kwa ajili ya: Malipo ya awali ya mkandarasi; Ujenzi wa miundombinu wezeshi; na njia (*Adit*) ya kufika kwenye mifereji mikubwa ya kuchepusha maji.

42. **Kuimarisha Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL):** Katika mwaka 2018/19 jumla ya shilingi bilioni 242.4 zilitengwa na kutumika kwenye maeneo yafuatayo: kukamilisha malipo ya ndege mpya aina ya Boeing 787-8 Dreamliner; kugharamia mafunzo ya marubani 79 na wahandisi wa ndege 88; ukarabati wa karakana ya ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro pamoja na kuanza taratibu za ununuzi wa ndege tatu mpya ambazo ni ndege moja aina ya Bombardier Q400 na ndege mbili aina ya Airbus A220-300. Kwa ujumla shilingi bilioni 746.6 zimetumika katika utekelezaji wa mradi huu na kuwezesha ndege mpya 11 kununuliwa ambapo ndege saba (7) zimepokelewa, ndege moja (1) inatarajiwa kupokelewa kabla ya mwisho wa mwaka 2019 na ndege tatu (3) zinaendelea kutengenezwa baada ya kulipwa kwa malipo ya awali.

43. **Miradi ya Umeme:** Mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa Msongo wa kV 220 Makambako – Songea umekamilika; na utekelezaji wa miradi ya kufua umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya nishati vikiwemo maji na gesi inaendelea. Miradi hiyo ni pamoja na: Mradi wa Kinyerezi I Extension – MW 185 (utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 85); Mradi wa Kufua Umeme wa Rusumo MW 80 (kuendelea kwa kazi ya kuchimba handaki la kupitishia maji na kukamilika kwa ujenzi wa barabara, kikinga maji, na nyumba za watumishi; na Mradi wa Kakono – MW 87 (kukamilika kwa kazi za utafiti wa kijiolojia na haidrolojia, usanifu wa awali na kuhushia tathmini ya athari za mazingira na kijamii). Aidha, hadi kufikia Septemba 2019 vijiji 8,102 kati ya vijiji 12,268 vya Tanzania Bara viliunganishwa umeme sawa na asilimia 66.4.

44. **Ujenzi wa Meli katika Maziwa Makuu:** Kukamilika kwa ujenzi wa meli ya MV Mbeya katika Ziwa Nyasa; na kuendelea na ujenzi na ukarabati wa meli katika Ziwa Victoria na Tanganyika. Jumla ya shilingi bilioni 564.7 zimetumika

45. **Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere:** Gharama za ujenzi wa jengo la tatu la abiria ilikuwa Euro milioni 276, sawa na takribani shilingi bilioni 722.1. Katika mwaka 2018/19, Serikali ilitumia jumla ya shilingi bilioni 92.2 kukamilisha ujenzi ambapo kazi zilizofanyika ni kuunganisha umeme wa gridi ya taifa katika jengo la III na kuweka mifumo

wezeshi ya TEHAMA. Jengo hilo lenye uwezo wa kuhudumia abiria milioni sita kwa mwaka limekamilika na limeanza kutumika. Aidha, ujenzi na ukarabati wa kiwanja cha ndege Mwanza umefikia asilimia 95 na shilingi bilioni 73 zimetumika. Vile vile, ujenzi na ukarabati wa viwanja vya mikoa upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambapo jumla ya shilingi bilioni 147.2 zimetumika.

46. **Ufungaji wa rada za kuongozea ndege za kiraia:** Hatua iliyofikiwa ni: **JNIA:** Kukamilika kwa miundombinu ya rada; na kukamilika kwa ufungaji wa mtambo; **Mwanza:** kukamilika kwa ujenzi wa Miundombinu ya Rada; kukamilika kwa ufungaji wa mtambo wa Rada; na kuendelea kwa majaribio ya mitambo. **KIA:** kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya Rada; kukamilika kwa ufungaji wa mitambo; na kuendelea kwa majaribio ya mitambo. **Songwe:** Ujenzi wa miundombinu ya majengo unaendelea. Aidha, ufungaji wa rada mbili ndogo unaendelea katika viwanja vya ndege vya Arusha na Zanzibar. Jumla ya shilingi bilioni 67.3 zimetumika.

47. **Uendelezaji wa Bandari:** katika bandari ya Dar es Salaam utekelezaji unaendelea ambapo gati Na.1 na Na. 2 yamekamilika, uboreshaji wa gati Na. 3 umefikia asilimia 60 na ujenzi wa gati la Ro-Ro umefikia asilimia 90. Uendelezaji huu umegharimu shilingi bilioni 180.56. Aidha, uboreshaji wa bandari za Tanga na Mtwara unaendelea ambapo shilingi bilioni 50 zimetumika. Vile vile, uboreshaji wa bandari za maziwa makuu unaendelea na umegharimu shilingi bilioni 3.5.

48. **Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania):** kukamilika kwa tathmini ya fidia kwa maeneo yatakayojengwa miundombinu wezeshi na kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali. Jumla ya shilingi bilioni 1.2 zimetumika katika kugharamia mradi huu.

49. **Ujenzi wa Barabara za Juu jijini Dar es Salaam:** kukamilika kwa ujenzi wa Mfugale Flyover na kuanza kutumika ambapo shilingi bilioni 96 zilitumika. Vile vile, ujenzi wa *Interchange* ya Ubungo umefikia asilimia 55 na shilingi bilioni 47.26 zimetumika.

50. **Ujenzi wa Barabara na Madaraja Makubwa:** kujengwa km 140.42 za barabara kuu na km 20.98 za barabara za mikoa kwa kiwango cha lami. Aidha, kwa upande wa madaraja hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa daraja la Sibiti (Singida), Momba (Rukwa) Mlalakuwa (Dar es Salaam), na Lukuledi (Lindi); kuendelea na ujenzi wa madaraja ya Mara (Mara) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98, Ruhuhu (Ruvuma) asilimia 80, Mangara (Manyara) asilimia 79 na ujenzi wa daraja jipya la Selander (Dar es Salaam) na daraja la Kigongo - Busisi (Mwanza) unaendelea. Jumla ya shilingi trilioni 2.2 zimetumika kugharamia miradi hiyo. Vile

vile, ujenzi wa barabara ya Morogoro sehemu ya Kimara – Kibaha kwa njia nane unaendelea ambapo shilingi bilioni 10 zimetumika

51. **Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi:** Shamba la Mkulazi I: kazi zilizofanyika ni pamoja na: kupatikana kwa kibali cha kutumia maji ya mto Ruvu; kukamilika kwa michoro kwa ajili ya ujenzi wa bwawa la maji lenye ukubwa wa mita za ujazo milioni 15 na maandalizi ya eneo kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda. Shamba la Mbigiri – Mkulazi II hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa eneo la mradi; kuendelea na ujenzi wa majengo ya kiwanda cha sukari; kuboresha miundombinu ya barabara na majengo; na kupatikana kwa mzabuni wa kutengeneza na kufunga mitambo ya kiwanda. Jumla ya shilingi bilioni 15.65 zimetumika katika kugharamia mradi huu.

52. **Miradi ya Kilimo:** Sekta ya kilimo iliendelea kuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa (asilimia 28.2). Jumla ya shilingi bilioni 56.5 zilitumika kwa mwaka 2018/2019 sawa na asilimia 45.6 ya makadirio ya shilingi bilioni 123.9. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kama ifuatavyo:

- (a) **Pembejeo za Kilimo na Uzalishaji wa Chakula:** Upatikanaji wa mbegu bora na mbolea ulikuwa tani 49,040.66 na tani 212,288.00 mtawalia. Aidha, jumla ya lita 296,000 na kilo 3,000 za kemikali za kilimo zilinunuliwa kwa ajili ya kudhibiti mlipuko wa magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao. Uzalishaji wa chakula ulifikia jumla ya tani 16,891,974 ikilinganishwa na mahitaji ya taifa ya chakula ya tani 13,569,285 sawa na ziada ya tani 3,322,689. Kati ya hizo, tani 9,537,857 zilikuwa za mazao ya nafaka na tani 7,354,117 zilikuwa za mazao yasiyo ya nafaka. Vile vile, Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ilinunua na kuhifadhi jumla ya tani 47,114.047 ili kuhakikisha upatikanaji wa chakula na udhibiti wa mabadiliko ya bei za mazao.
- (b) **Vyama vya Ushirika:** Idadi ya vyama vya ushirika iliongezeka kutoka 10,990 mwaka 2017/18 hadi kufikia vyama 11,331 mwaka 2018/19. Aidha, idadi ya wanachama iliongezeka kutoka 2,619,311 hadi kufikia 3,998,193 katika kipindi hicho. Mazao yaliyokusanywa na kuuzwa kupitia vyama vya ushirika chini ya mfumo wa stakabadhi ghalani yalikuwa: kahawa tani 97,151; korosho tani 224,824.4; chai tani 34,010; tumbaku tani 60,552.7; pamba tani 221,619 na kakao tani 4,445.6. Vile vile, kwa kutumia mfumo rasmi wa masoko ya mazao ya kilimo ulioanzishwa, jumla ya tani 333,227.4 za parachichi, ndizi, mbegu za kakao, mpunga, maharage, mahindi, mchele na vitunguu saumu ziliuzwa nje ya nchi.

- (c) **Mifugo:** Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuimarishwa kwa mashamba matano ya kuzalisha mitamba ya Sao Hill, Kitulo, Ngerengere, Nangaramo na Mabuki; kusambazwa kwa mitamba ya ng'ombe wa maziwa 15,097; Ununuzi na usambazaji wa lita 8,823.53 za viuatilifu vya kuulia kupe kwa ajili ya majosho 1,409 nchi nzima; kuongezeka kwa ng'ombe wa maziwa kutoka 1,100,000 mwaka 2017/18 hadi ng'ombe 1,294,882 mwaka 2018/19 ambapo uzalishaji wa maziwa umeongezeka kwa asilimia 6.67 kutoka lita bilioni 2.4 hadi kufikia lita bilioni 2.7; na usindikaji wa maziwa umeongezeka kutoka lita milioni 56 na kufikia lita milioni 66.9 mwaka 2018/19 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 19.4. Mafanikio mengine ni: jumla ya kilo 5,384,735.8 za ngozi ghafi zilizosindikwa kufikia hatua ya kati (*wet blue*) na bidhaa za ngozi zenye thamani ya shilingi milioni 8,165.4 zimeuzwa nje ya nchi; kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika viwanda vya utengenezaji wa chanjo na uchakataji wa mifugo na mazao yake ambapo viwanda 6 vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi; na wataalamu 889 walipatiwa mafunzo ya uhamilishaji mwaka 2018/19 ikilinganishwa na 204 mwaka 2017/18 sawa na asilimia 190.7.
- (d) **Uvuvi:** jumla ya tani 51,718.8 za samaki na mazao mengine ya samaki zenye thamani ya shilingi bilioni 691.8 ziliuzwa nje ya nchi; kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari ya uvuvi; kufanyika kwa operesheni 106 za doria za baharini na nchi kavu ambapo watuhumiwa 260 walikamatwa; kufanyika kwa kaguzi 401 za samaki na mazao ya samaki, viwanda vya samaki, vyumba vya kuhifadhia samaki katika hali ya ubaridi na stoo; na kuongezeka kwa maduhuli kutoka shilingi bilioni 21.5 hadi shilingi bilioni 30.3 mwaka 2018/19 ambapo sehemu kubwa ilichangiwa na mrabaha wa mauzo ya mazao ya uvuvi nje ya nchi.

53. **Miradi ya Madini:** Kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini, mafanikio yafuatayo yalipatikana: kukamilika kwa kituo cha Mfano cha Lwamugasa; uanzishwaji wa masoko 28 ya madini na vituo 11 vya ununuzi wa madini; ujenzi wa vituo saba (7) vya mafunzo ya umahiri kwa wachimbaji wadogo vya Bariadi, Musoma, Bukoba, Mpanda, Chunya, Songea na Handeni ambapo vituo 4 vimekamilika na 3 vipo katika hatua za mwisho kukamilika; kufanikisha tafiti 6 katika vituo vya mfano vya uchakataji madini; na kuboreshwa kwa mfumo wa utoaji wa taarifa za madini na utolewaji wa leseni ambapo leseni 13,108 zilitolewa. Kufuatia maboresho hayo, mapato ya madini yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 337.7 (mrabaha na tozo shilingi bilioni 335.2 na vyanzo vingine shilingi bilioni 2.5), sawa na asilimia 108.7 ya lengo la makusanyo la shilingi bilioni 310.6. Aidha, Serikali iliokoa madini (karati 66.6 za almasi, kilo 320.4 za dhahabu na kilo 75,957.3 za vito) zenye thamani ya dola za Marekani 13,566,078.6 sawa na shilingi bilioni 30.9. Vile

vile, madini yenye thamani ya dola za Marekeni 311,989.5 sawa na shilingi bilioni 71 yalitaifishwa. Kadhalika, Serikali ilikamilisha majadiliano na Kampuni ya Barrick ambayo yamewezesha kuundwa kwa kampuni mpya ya *Twiga Mineral Cooperation* inayomilikiwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania (hisa asilimia 16) na kampuni ya Barrick (hisa asilimia 84) kwa ajili ya uendeshaji wa migodi ya North Mara, Buzwagi na Bulyanhulu.

54. **Miradi ya Maji:** Katika mwaka 2018/19, Serikali ilitoa shilingi bilioni 140.5 sawa na asilimia 82.6 ya makadirio ya shilingi bilioni 170 kupitia Mfuko wa Maji. Fedha hizo zilitumika katika kukamilisha ujenzi wa miradi 198 na hivyo kufanya jumla ya miradi iliyokamilika kufikia 1,659 ikiwa na vituo 86,780 vya maji vinavyofanya kazi vyenye uwezo wa kuhudumia watu 25,359,290. Miradi mingine ya maji iliyotekelezwa inajumuisha: mradi wa maji wa Same - Mwanga - Korogwe (asilimia 60) na mradi wa maji kwenye makao makuu ya mikoa mipya ya Njombe (asilimia 95), Songwe (asilimia 90) na Geita (asilimia 100). Aidha, Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya mwaka 2019 imetungwa na kuanzisha Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA). Miradi mingine iliyotekelezwa katika kipindi cha mapitio ni pamoja na: upanuzi na ukarabati wa miradi ya Kitaifa ambapo mradi wa Chalinze (asilimia 79.5), mradi wa Wanging'ombe (asilimia 90); ukarabati wa mradi wa maji Nachingwea (umekamilika); na mradi wa maji wa Ziwa Victoria ambapo ulazaji wa bomba la kusambaza maji kwenye miji ya Isaka, Tinde na Kagongwa umekamilika kwa asilimia 99. Kwa ujumla hadi Juni 2019 shilingi bilioni 714 zimetumika katika kugharamia miradi ya maji.

55. **Miradi ya Elimu:** Serikali imeendelea kutekeleza sera ya Elimumsingi Bila Ada ambapo, shilingi bilioni 249.7 zilitolewa katika mwaka 2018/19. Uandikishwaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza mwaka 2019 ulikuwa 1,670,919 ikilinganishwa na lengo la kuandikisha wanafunzi 1,618,875, sawa na ufanisi wa asilimia 103.2.1. Aidha, udahili wa wanafunzi wa kidato cha kwanza wa elimu ya sekondari uliongezeka kutoka wanafunzi 595,427 mwaka 2018 hadi kufikia wanafunzi 733,103 mwaka 2019. Mafanikio haya yametokana na utekelezaji wa sera ya Elimumsingi Bila Ada ambapo wanafunzi wote wenye sifa walidahiliwa na kusajiliwa katika mfumo. Vile vile, shilingi bilioni 29.9 zilitolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya vyumba vya madarasa 2,392 katika shule 1,001 za sekondari; shilingi bilioni 56.8 zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, mabwalo, mabweni, matundu ya vyoo, hosteli na visima vya maji na shule mpya nne (4) za msingi za mfano kupitia programu ya lipa kulingana na matokeo katika sekta ya elimu; na shilingi bilioni 35.2 zilitolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa 2,760 na matundu ya vyoo 670 kwenye shule za msingi.

56. Katika kuboresha miundombinu na upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, Serikali imetekeleza yafuatayo: kujenga nyumba mpya za wafanyakazi na ukarabati shule 10 kongwe za sekondari za Serikali kwa gharama ya shilingi bilioni 18.7; ujenzi wa nyumba 70 za wafanyakazi katika shule zisizofikika kwa urahisi kwa gharama ya shilingi bilioni 4.2; shilingi bilioni 3.1 zilitolewa kwa ajili ya taasisi za elimu ya juu na shule za sekondari nchini; shilingi bilioni 6.2 zilitolewa kwa ajili ya kugharamia ukarabati na ujenzi wa vyuo vya ualimu vya Mpuguso, Kitangali, Ndala, na Shinyanga; shilingi bilioni 20.9 zilitolewa kwa ajili ya kugharamia uchapishaji, usafirishaji na usambazaji wa vitabu vya kiada na kiongozi cha mwalimu kwa elimu ya msingi na sekondari; na shilingi bilioni 59.4 zilitolewa kwa ajili ya uendeshaji na kugharamia ukarabati wa karakana na majengo ya VETA.

57. Katika mwaka 2018/19, wanafunzi wa elimu ya juu walionufaika na mikopo walikuwa 123,566 ikilinganishwa na 122,623 mwaka 2017/18. Kiasi kilichotumika mwaka 2018/19 kilifikia shilingi bilioni 427.6 ikilinganishwa na shilingi bilioni 443.1 mwaka 2017/18. Kupungua kwa matumizi kumetokana na kuimarisha udhibiti wa vigezo vya usajili na utoaji wa mikopo kwa wanafunzi pamoja na kupitia upya vigezo vya tathmini ya mikopo ya wanafunzi. Vile vile, shilingi bilioni 11.9 zimetolewa kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu katika vyuo vikuu vya SUA, Mzumbe, Ardhi na Sayansi na Teknolojia Mbeya -MUST. Hadi Juni 2019 jumla ya shilingi trilioni 1.8 zimetumika katika kugharamia miradi mbalimbali ya elimu.

58. **Miradi ya Afya:** Katika kipindi cha mapitio, jitihada mbalimbali zilifanywa na Serikali kuboresha utoaji wa huduma za afya. Kutokana na jitihada hizo, mafanikio yafuatayo yalipatikana: ujenzi wa hospitali mpya 67 za Wilaya (shilingi bilioni 100.5) na kuanza kwa maandalizi ya ujenzi wa hospitali tatu (3) mpya za Uhuru (Dodoma), Wilaya ya Tunduma (Songwe) na Manispaa ya Ubungo (Dar es Salaam); kuboresha upatikanaji wa dawa muhimu na vifaa tiba (shilingi bilioni 121.6); ununuzi wa mashine ya *PET Scan* katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* (shilingi bilioni 14.5); utoaji wa huduma za kinga na chanjo kwa watoto walio chini ya umri wa mwaka mmoja umefikia asilimia 97 (shilingi bilioni 7.0); ununuzi wa vifaa vya tiba katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (shilingi bilioni 1.4); na huduma za Mama na Mtoto kuendelea kuboreshwa ambapo ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya (470) umefikia asilimia 98 kwa gharama ya shilingi bilioni 184.6. Jumla ya fedha zilizotumika kugharamia miradi mbalimbali ya afya hadi Juni 2019 ni shilingi trilioni 2.3.

59. **Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato:** Katika mwaka 2018/19 Serikali iliendelea na utekelezaji wa miradi 18 katika Halmashauri 16 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 22.6 kilitolewa. Utoaji wa fedha ulizingatia hati za madai kwa kazi zilizokamilika. Aidha, katika kipindi hicho, mradi mmoja (soko la kisasa la Mburahati) ulikamilika na kuanza kutoa huduma na miradi 17 iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

60. **Mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma na Vanadium, Titanium na chuma Liganga:** Hatua iliyofikiwa ni: kukamilika kwa utafiti wa kina kuhusu wingi, aina na thamani za madini katika miamba ya Liganga; na kukamilika kwa uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi. Jumla ya shilingi milioni 700 zimetumika katika kugharamia mradi huu.

61. **Kanda Maalum za Kiuchumi:** Eneo Maalum la Uwekezaji Kigoma: Kazi zilizotekelezwa ni: kukamilika kwa upembuzi yakinifu na Mpango Kabambe wa uendelezaji wa eneo na ugawaji wa viwanja kwa ajili ya kupewa wawekezaji; na kuendeleza miundombinu kwa kufungua barabara zenye jumla ya km 28.46 na kuweka alama za mipaka 106. Eneo Maalum la Uwekezaji Mtwara: kukamilika kwa usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa barabara yenye urefu wa km 2.7 kufika eneo la mradi; kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya maji na kukamilika kwa usanifu wa kina wa miundombinu ya barabara. Jumla ya shilingi bilioni 5.8 zimetumika katika kugharamia miradi hii.

62. **Miradi ya Viwanda:** Serikali inaendelea kutekeleza miradi ifuatayo: kuimarisha Shirika la Viwanda Vidogo – SIDO; kuimarisha Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC); ukarabati na upanuzi wa kiwanda cha ngozi na bidhaa za ngozi cha Karanga – Moshi; kuendeleza mradi wa Magadi Soda – Bonde la Engaruka, Arusha; kuendeleza Kongane ya Viwanda TAMCO – Kibaha; kuimarisha mradi wa Kuunganisha Matrekta TAMCO-Kibaha; kuimarisha Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (TIRDO); na kuimarisha Shirika la Uhandisi na Usanifu Mitambo (TEMDO). Kiasi cha shilingi bilioni 20 zimetumika katika kugharamia miradi hii.

63. **Changamoto na hatua za kukabiliana nazo:** utekelezaji wa bajeti ulikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kuwepo kwa mahitaji makubwa yasiyowiana na uwezo wa mapato; kutoongezeka kwa mapato ya kodi kama ilivyotarajiwa; uwepo wa misaada na mikopo nafuu yenye masharti yanayokinzana na mila na desturi za kitanzania; kutopatikana kwa misaada na mikopo kutokana na baadhi ya Washirika wa Maendeleo kutotimiza ahadi zao na mabadiliko ya viwango vya riba katika masoko ya fedha ya nje; na ukwepaji kodi kwa njia mbalimbali kama vile biashara ya magendo. Katika kukabiliana na changamoto hizi Serikali

itaendelea: kuimarisha ulipaji kodi wa hiari kwa kutekeleza Mpango wa Kusimamia Vihatarishi vya Mwitikio wa Ulipaji Kodi; kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya mashine za stakabadhi za kielektroniki kupitia matumizi ya Mfumo ulioboreshwa wa usimamizi wa mashine za stakabadhi za kielektroniki; kuendeleza majadiliano na Washirika wa Maendeleo na taasisi za fedha za nje; kukuza soko la fedha la ndani; na kuendelea kuwianisha mapato na matumizi.

SURA YA TATU

MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/21

3.1. Utangulizi

64. Sura hii inaainisha sera za kibajeti na makadirio ya mapato na matumizi katika muda wa kati. Kwa mujibu wa Kifungu cha 21(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 Serikali inawajibika kuandaa na kutekeleza sera wezeshi za kibajeti ili kuchochea uwekezaji, ukuaji wa uchumi na kuboresha ustawi wa wananchi. Sera mahsusi za kibajeti katika muda wa kati, zinalenga kufanikisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 - 2020/21 na vipaumbele mbalimbali vya Serikali.

3.2. Shabaha na Malengo ya Uchumi Jumla

65. Shabaha na malengo ya uchumi jumla ni kama ifuatavyo: Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.1 mwaka 2020 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 7.0 mwaka 2019; Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia 5.0 katika kipindi cha muda wa kati; Mapato ya ndani kufikia asilimia 14.8 ya Pato la Taifa mwaka 2020/21; Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa asilimia 21.7 ya Pato la Taifa mwaka 2020/21; Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) inakuwa chini ya asilimia 3.0 kuendana na makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

3.3. Misingi ya Uchumi Jumla

66. Misingi itakayozingatiwa kufikia shabaha za uchumi jumla ni pamoja na: Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama, utulivu na umoja hapa nchini na katika nchi jirani; kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya kimataifa; na hali nzuri ya hewa itakayowezesha uzalishaji wa chakula cha kutosha.

3.4. Sera za Mapato na Makadirio katika Muda wa Kati

3.4.1. Sera za Mapato ya Ndani

67. Sera za mapato ya ndani katika muda wa kati zinalenga kuongeza makusanyo kwa kuendelea:

- (i) Kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji ili kukuza biashara ndogo na za kati kwa ukuaji endelevu wa uchumi;
- (ii) Kuboresha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari na upanuzi wa wigo wa kodi;
- (iii) Kuimarisha usimamizi wa ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi pamoja na mapato ya ndani ya Halmashauri kwa kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA;

- (iv) Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato; na
- (v) Kuwianisha na kupunguza tozo na ada mbalimbali ili kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji.


3.4.2. Makadirio ya Mapato ya Ndani

68. Mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya Halmashauri yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 23,456.3 mwaka 2020/21 kutoka shilingi bilioni 23,045.3 mwaka 2019/20. Katika muda wa kati, mapato hayo yanakadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 8.8 hadi shilingi bilioni 27,759.3. Mchango wa mapato ya ndani katika bajeti yanakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 68.3 mwaka 2020/21 hadi asilimia 73.7 mwaka 2022/23.

69. Katika mwaka 2020/21, mapato ya kodi yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 4.3 hadi shilingi bilioni 19,761.2 kutoka shilingi bilioni 18,955.2 mwaka 2019/20. Katika muda wa kati, mapato ya kodi yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 8.9 hadi shilingi bilioni 23,419.3 mwaka 2022/23. Mapato ya kodi katika Pato la Taifa yanakadiriwa kuwa asilimia 12.5 katika muda wa kati.

70. Katika muda wa kati, Mapato Yasiyo ya Kodi yakijumuisha mapato ya Halmashauri yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 4,340.0 mwaka 2022/23 kutoka shilingi bilioni 3,695.1 mwaka 2020/21, sawa na ongezeko la asilimia 17.5. Mapato Yasiyo ya Kodi yakijumuisha mapato ya Halmashauri yanakadiriwa kuwa asilimia 2.3 ya Pato la Taifa katika muda wa kati.

Kielelezo Na. 3.1: Makadirio ya Mapato katika Muda wa Kati (Shilingi Bilioni)



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

71. Katika muda wa kati, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati mahsusi ya kiutawala ili kufikia malengo ya makusanyo ya mapato ya ndani. Mikakati hiyo ni pamoja na:

- (i) Kupanua wigo wa kodi kupitia ukusanyaji na matumizi ya taarifa kutoka vyanzo na kanzidata mbalimbali kuhusu taarifa za walipakodi wapya na kurahisisha uandikishaji kwa kutumia mfumo wa usajili walipakodi wa kielektroniki;
- (ii) Kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya mashine za stakabadhi za kielektroniki kupitia matumizi ya Mfumo ulioboreshwa wa usimamizi wa mashine za stakabadhi za kielektroniki;
- (iii) Kuimarisha ulipaji kodi wa hiari wa walipakodi kwa kutekeleza Mpango wa Kusimamia Vihatarishi vya Mwitikio wa Ulipaji Kodi;
- (iv) Kutekeleza Mfumo wa Dirisha Moja la Kielektroniki la Tanzania (TeSWs) ili kurahisisha upitishaji wa mizigo katika vituo vya mipaka pamoja na kupunguza gharama za kufanya biashara nchini;
- (v) Kuimarisha ukaguzi wa mipaka katika nchi kavu na majini kwa kuongeza ushirikiano baina ya taasisi za ulinzi na usalama nchini ili kupunguza tatizo la uingizaji haramu wa bidhaa pamoja na biashara haramu;
- (vi) Kuharakisha usambazaji wa Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG);
- (vii) Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji katika taasisi za Serikali ili kuhakikisha

- kuwa michango stahiki ya Mashirika kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali inawasilishwa kwa wakati;
- (viii) Kununua mashine za kukusanyia mapato ya ndani ili kuziwezesha Halmashauri zenye uwezo mdogo wa kukusanya mapato kuwa na mashine za kutosha kulingana na mahitaji;
 - (ix) Kuandaa na kutekeleza mkakati wa kuwezesha Halmashauri ambazo zinakusanya mapato chini ya uwezo; na
 - (x) Kuwajengea uwezo na kuimarisha mahusiano kwa maafisa wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma katika ukadiriaji na ukusanyaji wa mapato ya ndani.

3.5. Sera za Misaada na Makadirio katika Muda wa Kati

72. Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo Tanzania (*Development Cooperation Framework-DCF*) utaendelea kutumika kama nyenzo ya mahusiano kati ya Serikali na Wadau wa Ushirikiano wa Maendeleo. Hivi karibuni Serikali imesambaza Mpango Kazi wa utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo kwa Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuboresha mahusiano kati ya Serikali na Wadau wa Ushirikiano wa Maendeleo.

73. Katika muda wa kati, misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 1,268.6 mwaka 2020/21 na kuongezeka hadi shilingi bilioni 1,316.9 mwaka 2022/23, sawa na ongezeko la asilimia 3.8 kutoka mwaka 2020/21. Misaada ya Kibajeti (*General Budget Support- GBS*) inatarajiwa kuwa Shilingi bilioni 154.2 mwaka 2020/21 na kuongezeka hadi shilingi bilioni 160.0 mwaka 2022/23. Misaada ya Mifuko ya Pamoja ya Kisekta (*Basket Funds*) inatarajiwa kufikia shilingi bilioni 172.9 mwaka 2020/21 na kuongezeka hadi shilingi bilioni 179.5 mwaka 2022/23. Misaada ya miradi (*Project Funds*) inatarajiwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 977.4 mwaka 2022/23 kutoka shilingi bilioni 941.5 mwaka 2020/21.

3.6. Sera ya Kugharamia Nakisi ya Bajeti

74. Katika muda wa kati, Serikali itaendelea na mkakati wa kuhakikisha mikopo kwa ajili ya kugharamia nakisi ya bajeti inapatikana kwa gharama nafuu sambamba na usimamizi madhubuti wa vihatarishi pamoja na uendelezaji wa masoko ya fedha ya ndani. Mkakati wa Muda wa Kati wa Kusimamia Deni la Serikali wa mwaka 2018/19 – 2022/23, unatoa mwongozo wa Serikali wa kukopa ili kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na deni linalohimilika. Hivyo, Serikali itaendelea kukopa kutoka katika vyanzo vyenye masharti nafuu na ya kati hususan vyanzo vinavyotoa mikopo kwa utaratibu wa *Export Credit Agency (ECA)* pamoja na mikopo yenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ya kimkakati.

Vilevile, kwa upande wa mikopo ya ndani, hatifungani zote za Serikali zinatumiwa kugharamia bajeti, kipaumbele kitatolewa kwenye hatifungani za muda mrefu ili kurefusha mtiririko wa uivaji wa amana za Serikali.

75. Katika muda wa kati, nakisi ya bajeti inayojumuisha misaada inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 3,943.4 sawa na asilimia 2.5 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2020/21 ambapo jumla ya shilingi bilioni 2,355.3 zitagharamiwa na mikopo ya nje na shilingi bilioni 1,588.2 itagharimiwa na mikopo ya ndani sawa na asilimia 1.0 ya Pato la Taifa. Nakisi ya bajeti inatarajiwa kupungua hadi shilingi bilioni 1,615.6 sawa na asilimia 0.9 ya Pato la Taifa mwaka 2022/23.

3.6.1. Ukopaji kutoka Vyanzo vya Ndani


76. Ukopaji katika soko la ndani utaendelea kuwa chanzo muhimu cha kugharamia bajeti ya Serikali hususan utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa ukopaji katika soko la ndani hauathiri ukopaji wa sekta binafsi. Serikali itarejesha utaratibu wa kutoa hatifungani za alama (*benchmark bond*) ili kuendeleza soko la ndani la dhamana za Serikali. Hatifungani hizo zitawezesha kuelekeza mwenendo wa viwango vya riba, kuongeza ujazo wa hatifungani na hivyo kuzifanya zihitajike zaidi na wawekezaji, kuweka uwazi katika bei za hatifungani na kupunguza athari katika soko la fedha. Hivyo, baada ya muda utaratibu huu utaiwezesha Serikali kukopa kutoka vyanzo vya ndani kwa gharama nafuu zaidi. Vile vile, Serikali itaanzisha utaratibu wa wananchi kushiriki katika minada ya amana za Serikali kwa kutumia simu za viganjani pamoja na kutoa elimu kwa umma ili kupanua wigo wa wawekezaji.

3.6.2. Ukopaji kutoka Vyanzo vya Nje

77. Serikali itaendelea kutumia mikopo ya masharti nafuu kama chanzo muhimu cha kuziba nakisi ya bajeti. Aidha, mabadiliko ya sera za Mashirika ya Fedha ya Kimataifa yanaathiri upatikanaji wa mikopo nafuu, hivyo kuulazimu Serikali kukopa mikopo yenye masharti ya kibiashara ili kuziba upungufu huo. Mikopo yenye masharti ya kibiashara itaendelea kugharamia miradi ya maendeleo yenye matokeo makubwa ya kiuchumi hususan mikopo yenye masharti ya kati na mikopo ya kibiashara itakayopewa kipaumbele ni ya riba isiyobadilika (*fixed rate*) ili kuepuka athari za kubadilika kwa riba.

78. Mchanganuo wa makadirio ya bajeti katika muda wa kati umeoneshwa katika Kielelezo namba. 3.2 na Jedwali na. 3.1 hadi 3.4.

Kielelezo Na. 3.2: Mchanganuo wa Mapato na Mikopo Katika Muda wa Kati (2020/21 - 2022/23) (Shilingi Bilioni)



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

3.7. Sera za Matumizi na Makadirio katika Muda wa Kati

3.7.1. Sera za Matumizi


79. Sera za Matumizi katika muda wa kati zitajumuisha yafuatayo: -

- (i) Kuendeleza nidhamu ya matumizi ya fedha za umma;
- (ii) Kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele yatakayochochea ukuaji wa uchumi na kuhakikisha kuwa miradi inayoendelea inapewa kipaumbele kabla ya miradi mipya;
- (iii) Kudhibiti ulimbikizaji wa madeni;
- (iv) Kuongeza kasi ya matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Serikali; na
- (v) Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa kuendana na vigezo vya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

3.7.2. Makadirio ya Matumizi

80. Katika mwaka 2020/21 matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 34,360.2 sawa na asilimia 21.7 ya Pato la Taifa kutoka shilingi bilioni 33,105.4 mwaka 2019/20. Katika muda wa kati matumizi ya Serikali yanakadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 4.7 hadi shilingi bilioni 37,684.3 mwaka 2022/23 kutoka shilingi bilioni 34,360.2 mwaka 2020/21.


Kielelezo Na 3.3: Mwenendo wa Makadirio ya Matumizi katika Muda wa Kati (2020/21 – 2022/23) (Shilingi Bilioni)



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

81. Katika mwaka 2020/21, matumizi ya kawaida yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 4.7 hadi shilingi bilioni 21,660.7 sawa na asilimia 13.7 ya Pato la Taifa na kuongezeka kwa asilimia 9.6 hadi shilingi bilioni 23,741.6 mwaka 2022/23. Matumizi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa shilingi bilioni 12,699.4 mwaka 2020/21 sawa na asilimia 8.0 ya Pato la Taifa na kuongezeka hadi shilingi bilioni 13,942.7 mwaka 2022/23.

Kielelezo Na. 3.4: Makadirio ya Matumizi katika Muda wa Kati kwa Aina Kuu za Matumizi (Shilingi Bilioni)




Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

3.7.3. Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kiuchumi

82. Katika mwaka 2020/21, mishahara (ikijumuisha mishahara ya Taasisi na Mashirika ya Umma) inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 7,762.39 (sawa na asilimia 33.1 ya makadirio ya mapato ya ndani) na kukadiriwa kuongezeka hadi shilingi bilioni 8,187.0 mwaka 2022/23 (sawa na asilimia 29.5 ya makadirio ya mapato ya ndani). Malipo ya mtaji kwa deni la ndani na nje yanakadiriwa kuongezeka kutoka shilingi bilioni 5,691.8 mwaka 2020/21 hadi shilingi bilioni 6,992.5 mwaka 2022/23 sawa na ukuaji wa asilimia 22.9.

83. Katika muda wa kati malipo ya riba yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 6.8 hadi shilingi bilioni 3,042.7 mwaka 2022/23 kutoka shilingi bilioni 2,848.6 mwaka 2020/21. Katika kipindi hicho, matumizi katika bidhaa na huduma pamoja na ruzuku kwa taasisi za umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa yanatarajiwa kuwa shilingi bilioni 5,357.9 mwaka 2020/21 na kupungua hadi shilingi bilioni 5,280.5 mwaka 2022/23. Aidha, matumizi yaliyoelekezwa kwenye shughuli za uwekezaji/maendeleo yataongezeka kwa asilimia 9.8 katika muda wa kati mpaka shilingi bilioni 13,942.7 mwaka 2022/23 kutoka shilingi bilioni 12,699.4 mwaka 2020/21.

Kielelezo Na.3.5: Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kiuchumi katika Muda wa Kati (2020/21 -2022/23)



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

84. Katika muda wa kati matumizi yataelekezwa katika miradi ya kipaumbele inayoendelea ikiwa ni pamoja na: Mradi wa kufua umeme kwa nguvu ya maji MW


2,115 wa Julius Nyerere; ujenzi wa reli ya kati ya *Standard Gauge*; kuimarisha Shirika la Ndege la Taifa; kusambaza umeme vijijini; ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji; upanuzi wa Bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga; na ujenzi wa meli na vivuko katika maziwa makuu. Maeneo mengine ya matumizi ni pamoja na malipo ya deni la Serikali, malipo ya mishahara, utekelezaji wa miradi yenye kuzalisha mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, utoaji wa elimu msingi bila malipo, uchaguzi mkuu, ujenzi wa barabara za juu Ubungo, utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na utoaji wa madawa, vifaa tiba na vitendanishi.

3.7.4. Makadirio ya Matumizi Kisekta

85. Sehemu hii inaainisha makadirio ya matumizi kisekta kwa kuzingatia majukumu ya Serikali katika muda wa kati. Matumizi haya yameainishwa kufuatana na malengo ya kisekta kama Afya, Elimu, Ulinzi na Utawala. Katika muda wa kati, kiasi kikubwa cha rasilimali kimeelekezwa katika shughuli za kiutawala ambazo zinajumuisha shughuli za kugharamia Deni la Serikali, ikifuatiwa na sekta za Uchumi, Elimu, Ulinzi na Afya kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 3.6**. Maelezo zaidi ya Makadirio ya matumizi kisekta yanaoneshwa katika **Kiambatisho Na. 1**.

Kielelezo Na. 3.6: Makadirio ya Matumizi Kisekta

(Shilingi Bilioni)



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

Jedwali Na. 3.1: Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti katika Muda wa Kati
2020/21 – 2022/23

Makadirio ya Bajeti katika Kipindi cha Muda wa Kati 2020/21 -2022/23				
	Shilingi Milioni			
	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
	BAJETI ILIOYODHINISHWA	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI
Mapato ya Ndani (Ikijumisha Mapato ya Halmashauri)	23,045,338	23,456,326	25,639,666	27,759,288
Mapato ya Ndani	22,279,855	22,652,569	24,795,721	26,873,146
Mapato ya Kodi (TRA)	18,955,186	19,761,186	21,674,929	23,419,288
Mapato ya Yasiyo ya Kodi (TRA)	145,746	174,895	209,874	251,849
Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Taasisi na Mashirika)	3,178,922	2,716,488	2,910,918	3,202,009
Mapato ya Halmashauri	765,483	803,757	843,945	886,142
Jumla ya Matumizi	27,669,094	28,668,342	29,298,741	30,691,788
Matumizi ya Kawaida	15,420,492	15,968,908	16,040,221	16,749,080
Malipo ya Riba Nje	987,312	1,265,799	1,157,177	1,288,622
Malipo ya Riba Ndani	1,438,950	1,582,757	1,661,637	1,754,142
Mishahara	6,391,294	6,583,033	6,780,524	6,983,940
Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Jamii	1,255,971	1,299,181	1,321,802	1,441,846
Bidhaa/ Huduma/ Ruzuku	5,346,965	5,409,939	5,119,080	5,280,532
o/w Matumizi Mengineyo	2,512,098	2,610,240	2,573,877	2,704,428
Matumizi ya Maendeleo	12,248,602	12,527,633	13,258,521	13,942,708
Fedha za Ndani	9,737,739	9,991,584	10,634,604	11,206,238
Fedha za Nje	2,510,863	2,536,049	2,623,917	2,736,470
Nakisi ya Bajeti bila ya Kujumlisha Misaada	-4,623,756	-5,212,016	-3,659,076	-2,932,500
Misaada	1,208,523	1,268,592	1,310,879	1,316,920
Misaada ya Kibajeti	146,822	154,164	159,303	160,037
Misaada ya Maendeleo	896,987	941,479	972,862	977,345
Mifuko ya Kisekta	164,713	172,949	178,714	179,538
Nakisi ya Bajeti Ikijumisha Misaada	-3,415,233	-3,943,423	-2,348,196	-1,615,580
Jumla ya Nakisi	-3,415,233	-3,943,423	-2,348,196	-1,615,580
Kuziba Nakisi	3,415,233	3,943,423	2,348,196	1,615,580
Kuziba Nakisi Kutoka Nje	1,915,459	2,355,254	793,818	-77,232
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	125,990	315,239	317,871	323,433
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	1,414,416	1,385,137	1,434,642	1,541,714
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	34,746	36,483	37,699	37,873
Mikopo ya Kibiashara	2,316,404	2,802,120	1,883,680	1,197,900
Kulipa Mtaji Deni la Nje	-1,976,098	-2,183,725	-2,880,074	-3,178,151
Kuziba Nakisi Kutoka Ndani	1,499,774	1,588,169	1,554,379	1,692,812
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	3,460,218	3,508,116	3,650,337	3,814,392
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	-3,460,218	-3,508,116	-3,650,337	-3,814,392
GDPmp	146,153,713	158,217,177	171,749,525	186,892,567

Jedwali Na. 3.2: Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti Kwa Asilimia ya Pato Ghafi la Taifa katika Muda wa Kati 2020/21 – 2022/23

Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Pato Ghafi la Taifa kwa Kipindi cha Muda wa Kati 2020/21 -2022/23				
	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
	BAJETI ILYOIDHINISHWA	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI
Mapato ya Ndani (kijumuisha Mapato ya LGAs)	15.8%	14.8%	14.9%	14.9%
Mapato ya Ndani	15.2%	14.3%	14.4%	14.3%
Mapato ya Kodi (TRA)	13.0%	12.5%	12.6%	12.5%
Mapato ya Yasiyo ya Kodi (TRA)	0.1%	0.1%	0.1%	0.1%
Mapato Yasiyo ya Kodi (Wizara, Taasisi na Mashirika)	2.2%	1.7%	1.7%	1.7%
Mapato ya Halmashauri	0.5%	0.5%	0.5%	0.5%
Jumla ya Matumizi	18.9%	18.1%	17.0%	16.3%
Matumizi ya Kawaida	10.6%	10.1%	9.3%	9.0%
Malipo ya Riba Nje	0.7%	0.8%	0.7%	0.7%
Malipo ya Riba Ndani	1.0%	1.0%	1.0%	0.9%
Mishahara	4.4%	4.1%	3.9%	3.7%
Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Jamii	0.9%	0.8%	0.8%	0.8%
Bidhaa/ Huduma/ Ruzuku	3.7%	3.4%	3.0%	2.8%
o/w Matumizi Mengineyo	1.7%	1.6%	1.5%	1.4%
Matumizi ya Maendeleo	8.4%	8.0%	7.7%	7.5%
Fedha za Ndani	6.7%	6.4%	6.2%	6.0%
Fedha za Nje	1.7%	1.6%	1.5%	1.5%
Nakisi ya Bajeti bila ya Kujumlisha Misaada	-3.2%	-3.3%	-2.1%	-1.6%
Misaada	0.8%	0.8%	0.8%	0.7%
Misaada ya Kibajeti	0.1%	0.1%	0.1%	0.1%
Misaada ya Maendeleo	0.6%	0.6%	0.6%	0.5%
Mifuko ya Kisekta	0.1%	0.1%	0.1%	0.1%
Nakisi ya Bajeti Ikijumlisha Misaada	-2.3%	-2.5%	-1.4%	-0.9%
Jumla ya Nakisi	-2.3%	-2.5%	-1.4%	-0.9%
Kuziba Nakisi	2.3%	2.5%	1.4%	0.9%
Kuziba Nakisi Kutoka Nje	1.3%	1.5%	0.5%	0.0%
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	0.1%	0.2%	0.2%	0.2%
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	1.0%	0.9%	0.8%	0.8%
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	0.0%	0.0%	0.0%	0.0%
Mikopo ya Kibiashara	1.6%	1.8%	1.1%	0.6%
Kulipa Mtaji Deni la Nje	-1.4%	-1.4%	-1.7%	-1.7%
Kuziba Nakisi Kutoka Ndani	1.0%	1.0%	0.9%	0.9%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	2.4%	2.2%	2.1%	2.0%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	-2.4%	-2.2%	-2.1%	-2.0%
GDPmp	146,153,713	158,217,177	171,749,525	186,892,567

Jedwali Na. 3.3: Makadirio ya Bajeti katika Muda wa Kati 2020/21 - 2022/23

	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
	BAJETI ILYIYODHINISHWA	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI
I. JUMLA YA MAPATO	33,105,410	34,360,183	35,829,153	37,684,332
Mapato ya Ndani	22,279,855	22,852,569	24,795,721	26,873,148
Mapato ya Halmashauri	765,483	803,757	843,945	886,142
Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti	272,813	469,402	477,174	483,470
Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi	2,311,404	2,326,616	2,407,504	2,519,059
Mifuko ya Kisekta	199,460	209,432	216,414	217,411
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	3,460,218	3,508,116	3,650,337	3,814,392
Mikopo ya Ndani ya Kibiashara	1,499,774	1,588,169	1,584,379	1,692,812
Mikopo ya Nje ya Kibiashara	2,316,404	2,802,120	1,883,680	1,197,900
II. JUMLA YA MATUMIZI	33,105,410	34,360,183	35,829,153	37,684,332
MATUMIZI YA KAWAIDA	20,856,808	21,660,749	22,570,632	23,741,624
Mfuko Mkuu wa Serikali	9,721,127	10,367,288	11,245,306	12,051,430
Mishahara	7,558,974	7,762,389	7,971,674	8,187,001
Matumizi Mengineyo	3,576,707	3,531,072	3,353,652	3,503,192
MATUMIZI YA MAENDELEO	12,248,602	12,699,434	13,258,521	13,942,708
Fedha za Ndani	9,737,739	10,163,365	10,634,604	11,206,238
Fedha za Nje	2,510,863	2,536,049	2,623,917	2,736,470

Jedwali Na. 3.4: Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Pato la Taifa katika Muda wa Kati 2020/21 - 2022/23

	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
	BAJETI ILYIYODHINISHWA	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI
I. JUMLA YA MAPATO	22.7%	21.7%	20.9%	20.2%
Mapato ya Ndani	15.2%	14.3%	14.4%	14.4%
Mapato ya Halmashauri	0.5%	0.5%	0.5%	0.5%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti	0.2%	0.3%	0.3%	0.3%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi	1.6%	1.5%	1.4%	1.3%
Mifuko ya Kisekta	0.1%	0.1%	0.1%	0.1%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	2.4%	2.2%	2.1%	2.0%
Mikopo ya Ndani ya Kibiashara	1.0%	1.0%	0.9%	0.9%
Mikopo ya Nje ya Kibiashara	1.6%	1.8%	1.1%	0.6%
II. JUMLA YA MATUMIZI	22.7%	21.7%	20.9%	20.2%
MATUMIZI YA KAWAIDA	14.3%	13.7%	13.1%	12.7%
Mfuko Mkuu wa Serikali	6.7%	6.6%	6.5%	6.4%
Mishahara	5.2%	4.9%	4.6%	4.4%
Matumizi Mengineyo	2.4%	2.2%	2.0%	1.9%
MATUMIZI YA MAENDELEO	8.4%	8.0%	7.7%	7.5%
Fedha za Ndani	6.7%	6.4%	6.2%	6.0%
Fedha za Nje	1.7%	1.6%	1.5%	1.5%

Jedwali Na. 3.5: Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Bajeti Yote katika Muda wa Kati 2020/21 – 2022/23

	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
	BAJETI ILIYOIDHINISHWA	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI
I. JUMLA YA MAPATO	100%	100%	100%	100%
Mapato ya Ndani	67.3%	65.9%	69.2%	71.3%
Mapato ya Halmashauri	2.3%	2.3%	2.4%	2.4%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti	0.8%	1.4%	1.3%	1.3%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi	7.0%	6.8%	6.7%	6.7%
Mifuko ya Kisekta	0.6%	0.6%	0.6%	0.6%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	10.5%	10.2%	10.2%	10.1%
Mikopo ya Ndani ya Kibiashara	4.5%	4.6%	4.3%	4.5%
Mikopo ya Nje ya Kibiashara	7.0%	8.2%	5.3%	3.2%
II. JUMLA YA MATUMIZI	100%	100%	100%	100%
MATUMIZI YA KAWAIDA	63.0%	63.0%	63.0%	63.0%
Mfuko Mkuu wa Serikali	29.4%	30.2%	31.4%	32.0%
Mishahara	23%	23%	22%	22%
Matumizi Mengineyo	10.8%	10.3%	9.4%	9.3%
MATUMIZI YA MAENDELEO	37.0%	37.0%	37.0%	37.0%
Fedha za Ndani	29.4%	29.6%	29.7%	29.7%
Fedha za Nje	7.6%	7.4%	7.3%	7.3%

3.8. Vipaumbele katika Muda wa Kati

86. Katika muda wa kati, Serikali itaendelea kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21. Aidha, maeneo mengine ya kipaumbele yatajumuishwa uimarishaji na usimamizi wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato na ugharamiaji wa deni la Serikali.

87. Vile vile, Serikali itafanya mapitio ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kwa lengo la kupima mafanikio na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha utekelezaji wake. Mapitio hayo yatasaidia kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa, 2021/22 - 2025/26 utakaokuwa na dhima ya “Kujenga Uchumi Shindani Unaoongozwa na Mauzo Nje”.

3.8.1. Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda

88. Kipaumbele cha Serikali kitakuwa katika utekelezaji wa miradi ya kielelezo inayoendelea yenye matokeo makubwa katika ukuaji wa uchumi, kuzalisha ajira na

kupunguza umaskini. Miradi hiyo ni pamoja na: mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere; ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha "Standard Gauge", kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); kusomesha wataalam wengi katika fani na ujuzi adimu na maalum kwa maendeleo ya viwanda na watu; na ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania). Aidha, Serikali itaendelea kuimarisha sekta ya kilimo kwa kuboresha upatikanaji wa mbegu na pembejeo za kilimo pamoja na kujenga na kukarabati miundombinu ya umwagiliaji, maghala na masoko.

3.8.2. Maendeleo ya Watu

89. Vipaumbele katika eneo la maendeleo ya watu vitajumuisha:

- (i) **Maji na Usafi wa Mazingira:** Kuboresha usambazaji maji mijini na vijijini; na kusimamia vyanzo vya maji na kudhibiti ubora; na kuboresha miundombinu ya uondoaji na uhifadhi wa majitaka.
- (ii) **Afya:** Kuboresha vituo vya Afya, hospitali za wilaya, mkoa na rufaa za mkoa; kusimika vifaa na vifaa tiba vya kisasa katika hospitali zote maalum; kuboresha vituo vya mafunzo ili kuongeza ubora wa rasimali watu; na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Lishe;
- (iii) **Elimu:** Kuimarisha utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote; kuendelea kutoa elimu singi bila ada; kuboresha utoaji wa elimu ya ufundi; kuboresha ukaguzi na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika vyuo vya mafunzo ya ufundi na ualimu; kuboresha mazingira ya kufundisha na kufundishia; na kuongeza fursa za upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu;
- (iv) **Ajira na Uendelezaji wa Ujuzi:** Kuongeza fursa za ajira pamoja na kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; na kuhamasisha ari ya ubunifu na ujasiriamali; na
- (v) **Utawala bora na Huduma Kwa Wananchi:** kudumisha amani, ulinzi na usalama; kuimarisha mifumo na taasisi za utoaji haki; kuendeleza utawala bora na demokrasia; kupambana na rushwa; kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa huduma za kisheria kwa wananchi; kuendelea na ujenzi wa miundombinu na majengo ya ofisi katika Makao Makuu ya Serikali Dodoma; na ugharamiaji wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

3.8.3. Kuboresha Mazingira ya kufanya Biashara na Uwekezaji

90. Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji kwa kutekeleza mipango mbalimbali ikiwemo Mpango Kazi wa Kuboresha Mazingira ya Biashara. Maboresho hayo yatajumuisha: kuwianisha kodi na tozo; miundombinu ya reli, barabara, nishati, viwanja vya ndege na bandari; ununuzi na ukarabati wa meli za abiria na mizigo; ununuzi na ukarabati wa vivuko; kuimarisha mifumo ya TEHAMA; kuongeza wigo wa Mkongo wa Taifa; kuharakisha uondoaji

wa mizigo bandarini; na kuendelea kuimarisha mahusiano na sekta binafsi.

3.8.4. Kuongeza Ufanisi katika Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano

91. Serikali itaendelea kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa mpango na bajeti katika muda wa kati kwa kutekeleza Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 - 2020/21. Utekelezaji wa Mkakati huu utajumuisha: kuendelea kuboresha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini; kuendelea kujengea uwezo watumishi wanaohusika na ufuatiliaji na tathmini; kuendelea na jitihada za kupambana na rushwa katika utekelezaji wa miradi; kurasimisha sekta isiyo rasmi; na kuimarisha ushiriki wa wananchi katika utekelezaji wa Mpango.

SURA YA NNE

VIHATARISHI VYA KIBAJETI KWA MWAKA 2020/21

4.1. Utangulizi

92. Sura hii inaelezea tathmini ya vihatarishi vinavyoweza kusababisha kutofikiwa kwa malengo ya uchumi jumla na bajeti. Katika mwaka 2020/21, Serikali itaendelea kuchukua tahadhari na hatua stahiki za kupunguza athari zinazoweza kutokana na vihatarishi hivyo kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439.

4.2. Vihatarishi vya Uchumi Jumla

(a) Ukuaji wa Pato la Taifa

93. Kilimo ni sekta inayoongoza katika uchangiaji wa Pato la Taifa, ambapo mwaka 2018 ilichangia asilimia 28.2. Katika kuhakikisha kilimo kinaendelea kuwa na mchango mkubwa, Serikali itaendelea kuchukua tahadhari ili kukabiliana na vihatarishi vinavyoweza kuathiri malengo ya ukuaji wa Pato la Taifa. Vihatarishi hivyo ni pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi, mlipuko wa magonjwa na wadudu wanaoharibu mazao, mabadiliko yasiyotarajiwa ya hali ya masoko ya bidhaa za kilimo na mabadiliko ya bei za pembejeo katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

(b) Mabadiliko ya Viwango vya Kubadilisha Fedha

94. Uimara wa sarafu ni muhimu katika kubaini gharama halisi za ulipaji wa madeni ya nje na gharama za uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi katika mwaka 2020/21. Deni la nje ni takribani asilimia 72 ya deni la Serikali, hivyo, endapo sarafu ya Tanzania itashuka thamani kwa kiwango kikubwa dhidi ya sarafu nyingine za nje, gharama za kulipa deni la nje zitaongezeka. Vilevile, gharama za kutekeleza miradi ya maendeleo zitaongezeka kutokana na baadhi ya mitambo, zana na vifaa kuagizwa nje ya nchi.

(c) Mabadiliko ya Bei za Bidhaa

95. Kushuka kwa bei ya dhahabu na bidhaa asilia zinazouzwa nje ya nchi kunaweza kupunguza mapato yanayotokana na mauzo nje ya nchi na hivyo kuongezeka kwa nakisi katika akaunti ya biashara na kupunguza akiba ya fedha za kigeni. Aidha, kuongezeka kwa bei za bidhaa kutoka nje hususan bidhaa za mafuta kunaweza kuongeza gharama za kupata bidhaa na huduma na hivyo kusababisha kushindwa kufikia malengo ya mapato na matumizi katika mwaka 2020/21.

4.3. Vihatarishi vya Bajeti

(a) Misaada na Mikopo

96. Misaada na mikopo ya nje na ndani ni miongoni mwa vyanzo vya kugharamia bajeti ya Serikali. Upatikanaji wa misaada na mikopo hutegemea hali ya uchumi na masharti ya taasisi za kifedha na nchi washirika wa maendeleo. Hali isiyotabirika ya utoaji wa misaada na mikopo hiyo na mabadiliko yasiyotarajiwa ya viwango vya riba katika masoko ya fedha ya ndani na ya kimataifa yanaweza kuathiri utekelezaji wa bajeti.

(b) Madeni Sanjari

97. Madeni sanjari yanaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Madeni sanjari yanayotokana na udhamini wa mikopo kwa Mashirika na Taasisi za Serikali pamoja na amri ya mahakama yanaweza kusababisha ongezeko la mahitaji yasiyotarajiwa ya matumizi na kuongeza nakisi ya bajeti. Aidha, tathmini isiyotosheleza ya madeni sanjari inaweza kuisababishia Serikali madeni makubwa yasiyotarajiwa katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

(c) Majanga ya Asili

98. Vihatarishi vinavyotokana na mabadiliko ya hali ya hewa hususan mafuriko, ukame, maporomoko ya ardhi, matetemeko na majanga mengine ya asili husababisha kukwama kwa shughuli za kiuchumi, uharibifu wa miundombinu na uhaba wa bidhaa na huduma. Aidha, uharibifu wa miundombinu unaweza kusababisha athari nyingine za kiuchumi zikiwemo kuongezeka kwa mfumuko wa bei, kuongezeka kwa gharama za uzalishaji viwandani; kupungua kwa faida za kampuni na hivyo kusababisha upungufu katika ukusanyaji wa mapato na kuongezeka kwa nakisi ya bajeti.

(d) Fidia, Ajali na Upotevu wa Mali

99. Madai yasiyotarajiwa ya fidia, ajali na potevu za mali zilizosababishwa na moto, wizi, udanganyifu na majanga ya asili husababishia Serikali matumizi ya ziada yaliyopo nje ya bajeti pamoja na ongezeko la deni la Serikali, na baadaye kuathiri utekelezaji wa bajeti ya Serikali. Aidha, uharibifu wa mali husababisha Serikali kushindwa kufikia malengo na shabaha iliyojiwekea katika kusimamia bajeti.

4.4. Hatua za Kukabiliana na Vihatarishi

100. Serikali itaendelea kutekeleza hatua za kukabiliana na vihatarishi ili kufikia malengo ya uchumi jumla. Hatua hizo ni pamoja na kutekeleza: Mwongozo wa Uandaaji wa Muundo wa Usimamizi wa Vihatarishi; Muundo wa Usimamizi wa Maafa unaoelekeza utaratibu wa kupunguza majanga hatarishi; na Mkakati wa

Madeni ambao unaiwezesha Serikali kubaini vihatarishi vikuu vya madeni.

101. Hatua nyingine ni pamoja na kuongeza jitihada katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ili kupunguza utegemezi katika misaada ya nje; kuimarisha utendaji wa Soko la Bidhaa (*Tanzania Mercantile Exchange-TMX*); kuhamasisha matumizi ya bima ya kilimo ili kukinga wakulima dhidi ya mabadiliko yasiyotarajiwa ya bei za mazao; na kuzingatia Sheria ya Bajeti, Sura 439. Aidha, Serikali inakamilisha Mwongozo wa Sera ya Usimamizi wa Mali na Mkakati wa Utekelezaji wenye lengo la kuongeza ufanisi na kuboresha usimamizi wa mali ya umma. Ukamilishaji wa mwongozo huo utaiwezesha Serikali kuandaa sheria na kanuni mahsusi zitakazotoa maelekezo ya usimamizi bora wa mali ya umma katika hatua mbalimbali za upatikanaji wa mali hizo, uingizaji wa taarifa za mali katika daftari, matumizi yake, utunzaji na matengenezo, uhasibu wa mali pamoja na uondoshaji wake.

102. Vile vile, Serikali itahakikisha Kamati za Maafa za Mikoa, Wilaya na Tarafa zinaandaa mipango na mikakati mbalimbali ya kuepusha na kukabiliana na maafa. Aidha, idhini ya kuhalalisha ununuzi wa mali mpya kufidia upotevu au uharibifu uliosababishwa na maafa, itatolewa baada ya kuwa na uthibitisho wa kutosha kuwa ununuzi huo ulifanyika kutokana na tukio la dharura. Tukio la dharura litahusisha tishio dhidi ya upotevu wa uhai kwa viumbe hai, ustawi au usalama na ulinzi wa raia ukihusisha majanga asilia, milipuko ya magonjwa, machafuko na vita kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Bajeti, Sura 439.

MATUMIZI YALIYOAINISHWA KISEKTA KWA MAJUKUMU YA SERIKALI

No.	SEKTA	SEKTA NDOGO	2020/21	2021/22	2022/23
1	Elimu		4,682,796.70	4,882,996.03	5,135,830.15
	1.1	Elimu Msingi	3,433,645.08	3,580,440.57	3,765,830.34
	1.2	Elimu ya Ufundi na Mafunzo	64,948.63	67,725.32	71,232.03
	1.3	Elimu ya Juu	894,323.74	932,557.94	980,844.37
	1.4	Sayansi na Teknolojia	63,217.37	65,920.05	69,333.29
	1.5	Huduma za Utawala katika Elimu	226,661.89	236,352.16	248,590.11
2	Afya		1,891,552.76	1,972,420.59	2,074,549.53
	2.1	Huduma za Tiba	520,324.93	542,569.91	570,663.35
	2.2	Huduma za Kinga	376,602.34	392,702.88	413,036.44
	2.3	Hospitali za Rufaa	125,038.15	130,383.79	137,134.87
	2.4	Zahanati	192,197.73	200,414.58	210,791.74
	2.5	Vituo vya Afya	177,975.26	185,584.07	195,193.33
	2.6	Hospitali za Wilaya	425,957.38	444,167.94	467,166.28
	2.7	Huduma za Utawala katika Afya	73,456.97	76,597.41	80,563.51
3	Huduma za Utawala na Deni la Taifa		12,920,169.44	13,472,533.65	14,170,120.97
	3.1	Mihimili ya Serikali na Utawala	2,300,375.20	2,398,721.05	2,522,923.18
	3.2	Fedha na Bajeti	2,286,127.71	2,383,864.44	2,507,297.32
	3.3	Mambo ya Nje	173,078.26	180,477.72	189,822.58
	3.4	Ugharamuaji wa Deni la Taifa	8,160,588.26	8,509,470.44	8,950,077.89
4	Ulinzi na Usalama wa Raia		3,073,203.41	3,204,589.27	3,370,518.03
	4.1	Ulinzi	1,922,889.55	2,005,097.09	2,108,917.97
	4.2	Usalama wa Raia	950,737.94	991,383.97	1,042,716.33
	4.3	Sheria na Mahakama	199,575.92	208,108.20	218,883.73
5	Shughuli za Kiochumi		9,016,862.40	9,402,352.09	9,889,191.59
	5.1	Kilimo	564,570.69	588,707.26	619,189.63
	5.2	Madini	51,301.77	53,495.03	56,264.92
	5.3	Nishati	2,223,982.21	2,319,062.09	2,439,139.60
	5.4	Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano	5,728,677.88	5,973,590.82	6,282,894.27
	5.5	Maliasili, Mazingira na Utalii	115,542.63	120,482.32	126,720.71
	5.6	Viwanda	85,976.26	89,651.92	94,293.97
	5.7	Biashara	212,903.24	222,005.30	233,500.39
	5.8	Kazi, Maendeleo ya Vijana na Kukuza Uuzi	33,907.73	35,357.35	37,188.10
6	Hifadhi ya Jamii		1,937,851.79	2,020,699.00	2,125,327.72
	6.1	Wazee, Watoto na watu wenye Ulemavu	20,686.37	21,570.76	22,687.66
	6.2	Mifuko ya Hifadhi ya Jamii	1,678,941.91	1,750,720.18	1,841,369.81
	6.3	Mfuko wa Bima ya Afya	238,223.50	248,408.05	261,270.24
7	Maji, Makazi na Maendeleo ya Jamii		837,746.49	873,561.90	918,793.60
	7.1	Maji	686,146.22	715,480.41	752,526.90
	7.2	Ardhi, Nyumba na Makazi	70,767.61	73,793.07	77,613.96
	7.3	Maendeleo ya Jamii	48,786.92	50,872.66	53,506.77
	7.4	Habari, Michezo na Utamaduni	32,045.74	33,415.76	35,145.98
	Jumla Kuu		34,360,182.99	35,829,152.52	37,684,331.59

**TAARIFA YA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA WIZARA/IDARA KWA
MWAKA 2018/19**

FUNGU	WIZARA/IDARA/WAKALA	Shilingi Milioni		
		BAJETI ILIYODHINISHWA	MAKUSANYO HALISI	ASILIMIAYA UFANISI
7	Ofisi ya Msajili wa Hazina	597,769.71	682,330.53	114.1%
14	Mambo ya Ndani - Jeshi la Zimamoto	9,250.00	6,219.60	67.2%
23	Wizara ya Fedha na Mipanga- Mhasibu Mkuu wa Serikali**	13.92	14,303.46	102734.4%
28	Mambo ya Ndani - Jeshi la Polisi	84,687.90	101,157.28	119.4%
29	Mambo ya Ndani- Magereza	1,800.00	2,205.90	122.5%
34	Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa	28,564.16	24,995.41	87.5%
37	Ofisi ya Waziri Mkuu - Mpiga Chapa wa Serikali	1,000.00	1,360.33	136.0%
40	Mfuko wa Mahakama	12,132.61	10,604.32	87.4%
43	Kilimo	2,315.01	2,394.88	103.4%
45	Ofisi ya Ukaguzi ya Taifa	765.68	836.46	109.2%
46	Elimu, Sayansi na Ufundi	163,942.89	177,135.49	108.0%
48	Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	120,000.00	97,223.99	81.0%
49	Maji na Umwagiliaji	5,119.00	5,713.14	111.6%
51	Mambo ya Ndani ya Nchi	926.61	94.39	10.2%
52	Afya na Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto (Afya)	19,775.50	18,913.18	95.6%
53	Maendeleo ya Jamii	3,090.80	2,075.72	67.2%
58	Nishati	394,450.86	579,803.39	147.0%
60	Viwanda, Biashara na Uwekezaji (Uwekezaji)	20,001.00	11,842.62	59.2%
62	Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano (Uchukuzi)	63,162.70	53,800.17	85.2%
64	Mifugo na Uvuvi (Uvuvi)	21,534.31	38,369.73	178.2%
65	Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu	38,882.85	29,276.42	75.3%
68	Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano (Mawasiliano)	15,010.29	35,282.88	235.1%
69	Maliasili na Utalii	23,631.11	15,548.10	65.8%
93	Mambo ya Ndani - Uhamiaji	200,350.11	170,695.78	85.2%
96	Habari, Michezo na Utamaduni	1,077.80	1,101.60	102.2%
99	Mifugo na Uvuvi (Mifugo)	18,467.95	33,730.57	182.6%
100	Madini	310,598.01	335,182.62	107.9%
	Wizara Nyingine na Mikoa	449.20	329.67	73.4%
	Jumla	2,158,770	2,452,527.60	

***Ufanisi wa Fungu 23 wa asilimia 102,734.4 ulitokana na makusanyo ya mishahara iliyorudishiwa (unclaimed salaries) ambayo kabla ya mwaka 2018/19, makusanyo hayo yalikuwa yakifanywa na mafungu husika. Kuanzia mwaka 2018/19, makusanyo hayo yanafanywa na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali.*

SEHEMU YA PILI

**MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA
2020/21**

UTANGULIZI

103. Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti (Mwongozo) umeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439. Mwongozo unatoa maelekezo ya jumla na mahsusi ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma wakati wa uandaaji na utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2020/21.

104. Katika kuandaa mpango na bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia Sera na Miongozo ifuatayo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 - 2020/21; Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015; Maelekezo ya Serikali yaliyoainishwa na Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi rasmi wa Bunge la 11 mwezi Novemba 2015; Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na Kanuni zake; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu; Malengo ya Maendeleo Endelevu; Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo; na makubaliano mengine ya kikanda na kimataifa ambayo Serikali imeyaridhia.

105. Sehemu ya Pili ya Mwongozo imegawanyika katika sura mbili. Sura ya Kwanza inatoa maelekezo ya kuzingatiwa katika kuandaa mpango na bajeti ya mwaka 2020/21; na Sura ya Pili inaainisha namna ya ujazaji wa fomu za uandaaji na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti. Sehemu hii itasomwa kwa pamoja na Sehemu ya Kwanza ya Mwongozo.

SURA YA KWANZA

MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/21

1.1. Uandaaji wa Mpango na Bajeti

106. Katika uandaaji wa Mpango na Bajeti, Maafisa Masuuli wanapaswa kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti na kubuni mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizopo kwenye Mafungu. Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga fedha kwa ajili ya mipango ya maendeleo na shughuli muhimu za uendeshaji wa ofisi ikiwemo shughuli za ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) pamoja na kulipa madeni ya watumishi, wazabuni na watoa huduma ili kuepuka ulimbikizaji wa madeni na gharama zitokanazo na riba na faini. Vile vile, Taasisi za Serikali zinazotarajia kupokea mikopo, misaada na dhamana zitapaswa kupata idhini kutoka kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha, kwa mujibu wa sheria.

1.2. Maandalizi ya Bajeti ya Mishahara

107. Wakati wa kuandaa ikama na bajeti ya mishahara kwa mwaka 2020/21, Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

- (i) Waraka wa Katibu Mkuu UTUMISHI kuhusu uandaaji wa ikama na makadirio ya bajeti ya mishahara kwa Mwaka 2020/21;
- (ii) Waraka wa Watumishi wa Serikali Na. 1 wa Mwaka 2015 na Waraka wa Msajili wa Hazina Na. 6 wa Mwaka 2015 kuhusu marekebisho ya mishahara na stahili za kisheria kwa watumishi wa Serikali na Taasisi za Serikali;
- (iii) Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu (2008), masuala ya Jinsia, VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa katika mpango na bajeti;
- (iv) Kujumuisha makisio ya nyongeza za mwaka za mishahara na upandishwaji vyeo katika bajeti ya mishahara kwa mwaka 2020/21; na
- (v) Kanuni D.51 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma, Toleo la Mwaka 2009 kuhusu upandishaji vyeo.

1.2.1. Kamati za Bajeti

108. Kamati za Bajeti katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma ni vyombo muhimu vya kuwashauri Maafisa Masuuli katika usimamizi wa bajeti kama ilivyoainishwa katika Kifungu 18(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439. Muundo wa Kamati hizi pamoja na majukumu yake yameainishwa katika Kifungu cha 17 (2) na

(3) cha Kanuni za Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015. Maafisa Masuuli wanapaswa kuhakikisha kuwa Kamati hizi zinafanya kazi ipasavyo wakati wa maandalizi na utekelezaji wa mpango na bajeti.

1.2.2. Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti

109. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma zinaelekezwa kuandaa mpango na bajeti ambayo ni shirikishi kwa kuzingatia Muundo wa Mapato na Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi. Mawasilisho hayo yanatakiwa kufanyika wiki ya tatu ya Januari 2020 baada ya kuidhinishwa katika ngazi za maamuzi husika ikijumuisha Mabaraza ya Wafanyakazi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma, Sura 105. Aidha, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatakiwa kuwasilisha Muundo wa Mapato na Matumizi OR-TAMISEMI; na Taasisi na Mashirika ya Umma kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina wiki ya pili ya Januari 2020 kabla ya kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango.

1.2.3. Uchambuzi wa Mpango na Bajeti

110. Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango nakala mango (*hard copy*) tano (5) na nakala tete (*soft copy*) ya makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu husika, siku tano (5) kabla ya kuanza uchambuzi ili kuwezesha mamlaka husika kufanya uchambuzi wa kina kwa ajili ya kuboresha mpango na bajeti. Aidha, Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kuwasilisha muhtasari wa makadirio ya mapato na matumizi katika nakala mango.

111. Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi utafanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, OR-TAMISEMI na Ofisi ya Msajili wa Hazina kuanzia tarehe 27 Januari hadi tarehe 7 Februari, 2020. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma wanatakiwa kuwasilisha nakala mango moja (1) na nakala tete Wizara ya Fedha na Mipango, OR-TAMISEMI na Ofisi ya Msajili wa Hazina baada ya uchambuzi.

112. Uchambuzi wa mpango na bajeti utafanyika kwa kuzingatia yafuatayo:

- (i) Taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2018/19;
- (ii) Taarifa ya mwenendo wa mapato na matumizi ya mwaka 2019/20 hadi kipindi cha nusu mwaka yakijumuisha changamoto na masuala muhimu

- yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa mpango na bajeti;
- (iii) Muundo wa uwasilishaji wa MTEF kwa mwaka 2020/21 hadi 2022/23 kama ilivyoainishwa kwenye Sura ya Pili ya Sehemu ya Pili ya Mwongozo;
 - (iv) Taarifa ya utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa vihatarishi kama ilivyoelekezwa katika Mwongozo wa Usimamizi wa Vihatarishi kwa Taasisi za Umma wa mwaka 2012;
 - (v) Vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 - 2020/21;
 - (vi) Viwango vya ukomo wa bajeti vilivyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;
 - (vii) Viwango vya ukomo wa bajeti wa Mifuko ya Pamoja ya Sekta vilivyooidhinishwa na kutolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;
 - (viii) Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2015 (PIM-OM) katika uandaaji wa miradi ya maendeleo;
 - (ix) Maelekezo ya Mwongozo, Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni za mwaka 2015, Nyaraka za Msajili wa Hazina pamoja na maelekezo mengine ya Serikali; na
 - (x) Utumiaji sahihi wa mageresho (*codes*) ya kibajeti (*Government Finance Statistics - GFS codes*) za mwaka 2014 wakati wa kuingiza takwimu.

113. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwasilisha miradi mipya inayotarajiwa kujumuishwa kwenye Bajeti ya mwaka 2020/21 mapema kabla ya wiki ya kwanza ya Januari 2020. Miradi itakayowasilishwa baada ya Januari 2020 itajumuishwa kwenye bajeti ya mwaka 2021/22 na 2022/23.

1.2.4. Majumuisho ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali

114. Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha Randama kwenye Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta kwa ajili ya uchambuzi na maboresho. Vikao vya Kamati za Bunge vitafanyika kuanzia tarehe 18 hadi 30 Machi, 2020. Baada ya uchambuzi wa Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta, Wizara ya Fedha na Mipango itafanya majumuisho ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Mafungu yote na kuchapisha vitabu kwa ajili ya kujadiliwa na kuidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1.2.5. Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep

115. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kukamilisha uingizaji wa takwimu sahihi za bajeti kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep kwa kuzingatia muda pamoja na masuala yafuatayo:

- (i) Usahihi wa makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2020/21 na makisio

ya miaka miwili inayofuata (2021/22 hadi 2022/23);

- (ii) Taarifa sahihi za Mpango Kazi na Mpango wa Mahitaji ya Fedha;
- (iii) Matumizi sahihi ya mageresho (*codes*) ya kibajeti na namba za miradi zinazotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;
- (iv) Matumizi sahihi ya vizio vya vipimo kama vilivyoainishwa kwenye mifumo ya CBMS na PlanRep; na
- (v) Ukadiriaji sahihi wa stahili za kisheria kama vile posho, pango, umeme, simu na maji kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa kuzingatia mabadiliko baada ya shughuli za Serikali kuhamishiwa Dodoma.

1.3. Mambo Mengine ya Kuzingatiwa katika Uandaaji wa Mpango na Bajeti

(a) Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu

116. Serikali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (2017 - 2022). Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

- (i) Kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa sekta ya umma na binafsi;
- (ii) Kuhakikisha kuwa mpango kazi wa kupambana na rushwa unajumuishwa kwenye mpango na bajeti kwa kila Fungu;
- (iii) Kuzijengea uwezo Taasisi na Kamati zinazohusika katika usimamizi wa mapambano dhidi ya rushwa; na
- (iv) Mapambano dhidi ya rushwa kuwa agenda ya kudumu katika Vikao vya Kisheria vya Wizara, Wakala, Taasisi za Serikali Zinazojitegemea, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(b) Programu ya Mabadiliko ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma Awamu ya Tatu (PSRP III).

117. Awamu ya tatu ya Programu ya Mabadiliko ya Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma imelenga kuboresha utoaji wa huduma kwa Umma na kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma ili kuboresha utendaji wa kazi. Maafisa masuuli wanaelekezwa kuzingatia mikakati ifuatayo katika mpango na bajeti: kuboresha maslahi kwa watumishi wa umma; kuimarisha nidhamu na uwajibikaji; kudhibiti rushwa; kupunguza urasimu na kuboresha utoaji wa huduma kwa umma. Vile vile, wakati wa uandaaji wa mpango na bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

- (i) Kuanzisha mipango ya motisha na kuweka misingi itakayoimarisha uwajibikaji;
- (ii) Kutumia mifumo ya kieletroniki katika utoaji wa huduma kwa umma ili

kuongeza ufanisi; na

- (iii) Kuimarisha usimamizi wa rasilimali watu kwa kuboresha taratibu za ajira, uteuzi, utoaji wa mafunzo elekezi, upandishaji vyeo na muda wa matazamio kwa kuzingatia sifa na vigezo.

(c) Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)

118. Utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ni miongoni mwa maeneo ya kipaumbele katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

- (i) Kusimamia kikamilifu matumizi endelevu ya maji na ardhi;
- (ii) Kuongeza tija na faida kwenye kilimo, mifugo na uvuvi;
- (iii) Kuimarisha upatikanaji wa masoko na kuongeza thamani kwenye mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi; na
- (iv) Kuweka mazingira wezeshi katika uwekezaji wa kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na tathimini.

(d) Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Awamu ya Tatu

119. Serikali inatarajia kutekeleza Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Awamu ya Tatu ili kuboresha usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Serikali katika ngazi ya Serikali za Mitaa. Aidha, Programu inalenga kuimarisha mahusiano ya kiutendaji kati ya Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

- (i) Kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maeneo ya uratibu, ufuatiliaji, tathmini na uandaaji taarifa;
- (ii) Kuweka mazingira wezeshi ya kuboresha shughuli za kiuchumi katika ngazi ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- (iii) Kujenga uwezo kwa watumishi wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maeneo ya utawala bora, elimu ya uraia, usimamizi wa fedha, mpango na bajeti, uandaaji na usimamizi wa miradi na rasilimali watu; na
- (iv) Kuimarisha shughuli za ushiriki wa jamii katika kutekeleza na kutoa maamuzi kuhusiana na masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa katika ngazi za msingi za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(e) Taasisi na Mashirika ya Umma

120. Serikali inaendelea kuboresha utendaji na usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma ili kuongeza ufanisi na tija. Ofisi ya Msajili wa Hazina imeandaa mikakati ya kuboresha utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma ili kuhakikisha yanaendeshwa kwa misingi na madhumuni ya uanzishwaji wake. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

- (i) Kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 10(A) cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2015 kwa kutenga na kuwasilisha kwa wakati katika Mfuko Mkuu wa Serikali michango ya asilimia 15 ya mapato ghafi;
- (ii) Kuimarisha mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa taasisi za Serikali na kampuni ambazo Serikali ina hisa ili kuongeza ufanisi na tija na kutoa michango/gawio stahiki Serikalini kwa wakati;
- (iii) Kuzingatia maelekezo ya Msajili wa Hazina yaliyotolewa kupitia Waraka wa barua yenye Kumb. Na. CEA. 170/344/01 ya tarehe 10 Julai 2019 kuhusu matumizi na mikutano ya Bodi za Wakurugenzi;
- (iv) Kubuni mikakati ya kuongeza vyanzo vya mapato ya ndani;
- (v) Kuandaa na kuwasilisha kwa Msajili wa Hazina mpango mkakati wa kuboresha utendaji wa mashirika ili kuepuka kujiendesha kwa hasara;
- (vi) Kutenga fedha kwa ajili ya kulipa malimbikizo ya madeni yanayotokana na gharama za huduma zilizotolewa na mashirika ya umma na watoa huduma binafsi;
- (vii) Kutumia mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi; na
- (viii) Kuandaa na kuwasilisha mikakati ya uwekezaji, mwongozo wa gawio na mipango ya biashara kwa Msajili wa Hazina kwa ajili ya kuidhinishwa.

(f) Upatikanaji wa Huduma za Fedha

121. Serikali inaendelea kutekeleza sera, mikakati na sheria kwa lengo la kujenga mfumo thabiti katika sekta ya fedha kwa ajili ya kuongeza ufanisi na upatikanaji wa rasilimali fedha kwenye shughuli za kuchochea ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma jumuiishi za fedha. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

- (i) Kutoa elimu ya fedha kwa umma kuhusu: huduma ya fedha zilizopo nchini; masoko ya mitaji na dhamana; soko la bidhaa; na fursa zilizopo katika taasisi za fedha za maendeleo;
- (ii) Kuimarisha taratibu za usajili wa hatimiliki za ardhi na mali;
- (iii) Kuanzisha na kuimarisha vituo vya kuendeleza biashara ndogo na za kati;
- (iv) Kujumuisha makundi ya watu wenye mahitaji maalum, jinsia na vijana katika upatikanaji na utumiaji wa huduma za fedha kwa usawa na gharama nafuu;
- (v) Kujumuisha masuala ya huduma za fedha katika mpango na bajeti za Mikoa na Halmashauri ikiwa ni pamoja na kuhuisha sheria ndogo za Mamlaka za Serikali za Mitaa; na
- (vi) Kuhamasisha matumizi ya teknolojia ya mawasiliano katika sekta ya fedha.

(g) Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi

122. Kifungu cha 7 (3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 kimerekebisha mwaka 2018

ili kujumuisha miradi inayotekelezwa kwa utaratibu wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi wakati wa maandalizi ya mpango na bajeti kama njia mbadala ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kwa mujibu wa Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi, Sura 103 (marejeo ya 2018) na Kanuni za mwaka 2015, Taasisi inayokusudia kutekeleza mradi wa ubia inatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango andiko la mradi na upembuzi yakinifu wa awali kila mzunguko wa bajeti unapoanza kama ilivyoainishwa kwenye vipaumbele vya Maendeleo ya Taifa kwa ajili ya uchambuzi.

123. Sheria ya Ubia, Sura 103 inaelekeza mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kutenga fedha kwa ajili ya kuandaa upembuzi yakinifu wa mradi wa ubia ikiwa ni pamoja na ushahidi kwamba kutekelezwa kwa mradi kwa utaratibu wa ubia utaleta thamani ya fedha zaidi ikilinganishwa na utekelezaji wa mradi kwa kutumia fedha za Serikali. Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma unaotaka kutoa kipaumbele kwa miradi ambayo haivutii uwekezaji wa Sekta Binafsi itekelezwe kwa utaratibu wa kawaida wa kibajeti.

(h) Usimamizi wa Mali za Umma

124. Serikali inaendelea kutoa miongozo inayolenga kutatua changamoto za sera, sheria, kanuni, utendaji na matumizi ya teknolojia katika kusimamia mali ya Umma. Katika kutekeleza azma hii, Serikali imetoa Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma wa mwaka 2019 pamoja na Waraka wa barua ya Mlipaji Mkuu wa Serikali yenye Kumb. Na. KA.32/244/01/53 wa tarehe 03/07/2019 unaoelekeza taratibu na mifumo katika kusimamia mali ya umma. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

- (i) **Usalama na Ulinzi wa Mali ya Umma:** Kuchambua na kutambua aina ya vihatarishi na kuandaa daftari la vihatarishi pamoja na kusimamia mikakati ya kuepuka majanga;
- (ii) **Ajali iliyohusisha Mali ya Umma:** Kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango, taarifa ya ajali iliyohusisha mali ya umma. Taarifa hiyo ijumuishe: Ripoti ya Ajali - TFN 80; Ripoti ya Awali ya Uchunguzi wa Jeshi la Polisi-PF - 90; Ripoti ya Ukaguzi wa Chombo cha Moto - PF 93 na Ripoti ya Gharama za Matengenezo. Aidha, taarifa nyingine zitakazowasilishwa ni pamoja na Hukumu ya Mahakama, Ripoti ya Jeshi la Polisi - PF 115 na Ripoti ya Hatua za Nidhamu zilizochukuliwa kwa mtumishi wa umma aliyesababisha ajali;
- (iii) **Ufutaji wa Potevu kwa Mali ya Umma:** Kuandaa na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango, taarifa ya potevu kwa mali ya umma pamoja na viambatisho vyake. Taarifa hiyo itawasilishwa kwenye Mamlaka ya Ufutaji

kwa kuzingatia Kanuni za Sheria ya Fedha za Umma 2004 (R.E). Aidha, viambatisho vitahusisha: Orodha ya Mali Chakavu – S.F 15 kwa mali zilizoharibika; Orodha ya Mali Pungufu – S.F 14 kwa mali zilizopotea kwenye vitabu; Ripoti Kamili ya Polisi na Hukumu ya Mahakama kwa potevu zitakazohusishwa na Wizi na Udanganyifu; na Ripoti ya Kamati ya Uchunguzi kwa potevu zilizosababishwa na moto au majanga asilia;

- (iv) **Mfumo wa Usimamizi wa Mali (GAMIS):** Kutenga rasilimali kwa ajili ya kugharamia mafunzo na kuunganisha mfumo wa GAMIS utakaorahisisha kazi ya kuhuisha taarifa ya mali ya umma kwa wakati; na
- (v) **Uhalalisho wa Ununuzi wa Mali ya Umma:** Kuomba uhalalisho wa ununuzi wa mali endapo kulitokea tukio la dharura. Dharura itahusisha matukio yanayotishia uhai wa viumbe hai, ustawi au usalama na ulinzi wa raia ukihusisha majanga asilia, milipuko ya magonjwa, machafuko na vita.

(i) **Matumizi ya Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG)**

125. Ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutumia Mfumo wa GePG ikiwa ni pamoja na kuhakikisha mapato kutoka vyanzo vyote yanakusanywa kupitia GePG kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Sura 348 na Kanuni za GePG za mwaka 2019.

(j) **Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato**

126. Katika mwaka 2020/21 Serikali itatoa kipaumbele katika ukamilishaji wa miradi ya kimkakati ambayo iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Maafisa Masuuli wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wenye miradi ya kimkakati inayoendelea wanaelekezwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi hiyo ili kuhakikisha kuwa inatekelezwa kwa ufanisi, kuzingatia thamani ya fedha na kukamilika kwa wakati.

(k) **Hatua za Kudhibiti Matumizi**

127. Maafisa Masuuli wanapaswa kusimamia nidhamu ya matumizi ya Fedha za Umma katika Taasisi wanazosimamia kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Aidha, hatua za kudhibiti matumizi zichukuliwe pasipo kuathiri ubora wa utoaji huduma. Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia yafuatayo: -

- (i) Kuhakikisha ununuzi wa umma unafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 na Kanuni zake ili kupata thamani halisi ya fedha iliyotumika, ununuzi wa pamoja na matumizi ya *Force Account*;
- (ii) Kuendelea na utaratibu wa kutumia Wakala ya Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) kwenye ununuzi wa magari baada ya kupata kibali kutoka

Ofisi ya Waziri Mkuu;

- (iii) Kutumia Mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (TANePS) katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi za ujenzi;
- (iv) Kutoingia mikataba bila kuwa na uhakika wa upatikanaji wa fedha ili kuepuka malimbikizo ya madai;
- (v) Kupunguza gharama na kuongeza ufanisi kwa kutumia TEHAMA katika mawasiliano Serikalini kama vile matumizi ya majalada ya kielektroniki;
- (vi) Kudhibiti safari za nje ya nchi na gharama zisizo na tija;
- (vii) Kutumia kumbi za Taasisi za Umma kwa semina, mafunzo, warsha na mikutano ya Bodi;
- (viii) Taasisi za umma zinaelekezwa kutumia hati za madai na mikataba ya watoa huduma wa ndani kuwa katika fedha za Kitanzania (Shilingi) ili kupunguza athari za mabadiliko ya viwango vya ubadilishaji fedha;
- (ix) Kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi hasa kwa bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani;
- (x) Kutumia vifaa vya teknolojia vinavyopunguza matumizi ya nishati; na
- (xi) Kuhakikisha gharama za miradi inayoendelea zinajumuishwa kwenye mpango na bajeti kabla ya kuanzisha miradi mipya.

(I) Usimamizi wa Fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi (D - Fund)

128. Katika kuhakikisha uwajibikaji na utunzaji wa hesabu kwa miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo kupitia utaratibu wa kupeleka fedha moja kwa moja kwa watekelezaji (D - Fund), Maafisa Masuuli wanatakiwa kupata idhini ya Wizara ya Fedha na Mipango kama ilivyoainishwa kwenye Waraka wa Hazina Na. 2 wa Mwaka 2019. Waraka huo unaelekeza utaratibu wa kuomba na kuhamisha fedha za Washirika wa Maendeleo kwenda moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuwasilisha orodha ya shughuli zitakazotekelezwa kwenye mradi.

(m) Ulipaji na Udhhibiti wa Ulimbikizaji wa Madeni

129. Kwa kuzingatia kifungu cha 52(2) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 kinachowataka Maafisa Masuuli kutenga fedha kwa ajili ya ulipaji wa madeni, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

- (i) Kuhakikisha madeni yote yamehakikiwa na Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali;
- (ii) Kuweka kipaumbele katika utengaji wa fedha za kulipia madeni yaliyohakikiwa kwa kutumia ukomo wa bajeti uliotolewa kwa mwaka 2020/21; na
- (iii) Kuhakikisha hakuna ulimbikizaji wa madeni mapya.

(n) Kiwango cha Ubadilishaji Fedha

130. Katika kuandaa mpango na bajeti katika mwaka 2020/21, makadirio yote ambayo yanatumia fedha za kigeni yatumie kiwango elekezi cha ubadilishaji fedha za kigeni kwa Shilingi za Tanzania cha Dola Moja ya Marekani kwa Shilingi za Tanzania 2,335.10.

(o) Kujumuisha Masuala Mtambuka katika Mpango na Bajeti

131. Serikali inaendelea kutekeleza na kujumuisha masuala mtambuka katika mpango na bajeti ili kupata matokeo chanya. Katika kufikia azma hiyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango ya masuala mtambuka ikijumuisha jinsia, mazingira, lishe, mabadiliko ya tabianchi, watu wenye ulemavu, wazee, ulinzi na haki za watoto, VVU/UKIMWI, utawala bora na utawala wa sheria.

(p) Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

132. Serikali inaendelea kutekeleza makubaliano na itifaki za mikataba iliyoridhiwa kikanda na kimataifa. Ili kushiriki kikamilifu na kunufaika na ushirikiano wa kikanda na kimataifa, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

- (i) Kuzingatia Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo;
- (ii) Kuingiza masuala ya ushirikiano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na masuala mengine ya mtangamano katika mpango na bajeti zao;
- (iii) Kuainisha na kutumia fursa za ugharamiaji wa shughuli za maendeleo zinazopatikana kikanda, nchi na nchi na kimataifa; na
- (iv) Kuwasilisha ahadi ya fedha zinazotarajiwa kutolewa na Washirika wa Maendeleo kupitia taasisi za kikanda na kimataifa ili kujumuishwa katika bajeti.

(q) Ugharamiaji wa Miradi Kupitia Fedha za Nje

133. Serikali inaendelea kushirikiana na Washirika wa Maendeleo katika kutekeleza programu na miradi ya maendeleo kwa kuzingatia Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo. Maafisa Masuuli wanaelekezwa:

- (i) Kuwasilisha ukomo wa bajeti za kissekta Wizara ya Fedha na Mipango (kwa Wizara zinazoratibu Mifuko ya Kissekta) kabla ya tarehe 31 Desemba 2019;
- (ii) Kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango katika kukamilisha ukomo wa ahadi za fedha za nje katika mafungu yao kabla ya tarehe 15 Januari 2020;
- (iii) Kuibua, kuandaa na kutathmini miradi kwa kuzingatia Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma;
- (iv) Kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi inayotekelezwa kwa ushirikiano na Washirika wa Maendeleo kwa mujibu wa makubaliano; na

- (v) Kuainisha kipengele cha msamaha wa kodi katika mikataba ya miradi inayostahili kupata msamaha.

1.4. Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

1.4.1. Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa

134. Katika kipindi cha maandalizi ya mpango na bajeti, Sekretarieti za Mikoa zinapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo:

- (i) Kusimamia na kudumisha masuala ya ulinzi na usalama katika maeneo ya utawala;
- (ii) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika maeneo yao ya utawala kwa kufanya Vikao vya Ushauri vya Wilaya na Mikoa pamoja na vikao vya Kamati za Usalama za Wilaya na Mikoa;
- (iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa katika mikoa na halmashauri;
- (iv) Kutambua maeneo ya mipaka na kuweka alama za mipaka ya Mikoa, Wilaya na Tarafa;
- (v) Kuhuisha Mipango Mikakati ya Mikoa, Wasifu wa Mikoa na Mikakati ya Maendeleo ya Kiuchumi ya Mikoa ili kuendana na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Vipaumbele vinavyoibuliwa kupitia utaratibu wa Fursa na Vikwazo vya Maendeleo ulioboreshwa mwaka 2019, Malengo ya Maendeleo Endelevu, Hati ya Mgawanyo wa Majukumu ya OR-TAMISEMI na kuweka kwenye Tovuti za Sekretarieti za Mikoa;
- (vi) Kutenga fedha za usimamizi wa utoaji huduma za jamii na kiutawala katika ngazi ya Halmashauri na ngazi ya vituo vya kutolea huduma za jamii;
- (vii) Kutenga fedha za ujenzi, ukarabati na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ofisi na Makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa Wilaya na Maafisa Tarafa, kipaumbele ni kutekeleza miradi inayoendelea kabla ya kuanza miradi mipya;
- (viii) Kufanya maandalizi na kuratibu shughuli za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020;
- (ix) Kuingiza takwimu za kibajeti kwenye mfumo wa CBMS kwa fedha za ruzuku ya uendeshaji wa kisekta katika Serikali za Mitaa kwa kutumia vifungu maalum vilivyoinishwa kwa ajili ya fedha za mishalaha, matumizi mengineyo na fedha za maendeleo;
- (x) Kuratibu utekelezaji wa shughuli za huduma ndogo za fedha katika ngazi ya Mkoa kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo ya Fedha ya Mwaka 2017 na Mkakati wa Utekelezaji wake pamoja na Sheria ya Huduma ndogo za Fedha Na. 10 ya Mwaka 2018;

- (xi) Kusimamia Serikali za Mitaa katika kubuni, kuandaa maandiko na kufuatilia utekelezaji wa miradi ikiwa ni pamoja na miradi ya ubia na vyanzo vingine vya mapato ya ndani;
- (xii) Kutenga fedha kwa ajili ya kuwajengea uwezo watumishi wa Sekretarieti za Mikoa ili kutoa ushauri wa kitaalam kwa watumishi wa Serikali za Mitaa;
- (xiii) Kutumia fedha za miradi zilizovuka mwaka wa fedha (2019/20) kabla ya Septemba 30 kwa mujibu wa Kifungu cha 29(3) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kifungu cha 21(3) cha Kanuni za Bajeti; na
- (xiv) Kupata idhini ya Wizara ya Fedha na Mipango kama ilivyoainishwa kwenye Waraka wa Hazina Na. 2 wa Mwaka 2019 kuhusu maelekezo ya kuomba na kuhamisha fedha za Washirika wa Maendeleo kwenda moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo (D - Fund) ikiwa ni pamoja na kuwasilisha orodha ya shughuli zitakazotekelezwa kwenye mradi.

1.4.2. Maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa

135. Katika maandalizi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2020/21, Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo:

A. Maelekezo ya jumla

- (i) Kusiimamia na kudumisha masuala ya Ulinzi na Usalama;
- (ii) Kufanya maandalizi na kuratibu shughuli za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020;
- (iii) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika maeneo ya utawala kwa kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na kuwezesha kufanyika kwa vikao vya kisheria vya Kamati za Maendeleo za Kata na mikutano ya Vijiji, Mitaa na Vitongoji;
- (iv) Kutenga asilimia kumi ya mapato yanayokusanywa kutoka kwenye vyanzo vya ndani vya Halmashauri kwa ajili ya kutoa mikopo kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa mujibu wa marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 (37A) na Kanuni zake za Mwaka 2019;
- (v) Kutenga fedha kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo kwa kuzingatia mwongozo wa OR-TAMISEMI unaozigawa Halmashauri kwenye madaraja kulingana na uwezo wa kukusanya mapato;
- (vi) Kuhakikisha kuwa mifumo ya kielekroniki inatumika katika makusanyo ya mapato, uandaaji wa mpango na bajeti, utoaji wa taarifa na usimamizi wa utoaji wa huduma za afya na elimu;
- (vii) Kupitia, kurekebisha na kuandaa Sheria Ndogo ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato na Utawala Bora katika ngazi ya Kijiji, Mtaa na Kitongoji; Kutenga fedha kwa ajili ya kuimarisha kamati za maafa katika ngazi za

- Wilaya, Kata na Kijiji/Mtaa kwa ajili ya kukabiliana na majanga asilia ikijumuisha utayari, mafunzo na uwepo wa vifaa katika maeneo ya utawala;
- (viii) Kutumia Mwongozo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo ulioboreshwa mwaka 2019 katika kuainisha vipaumbele vya maendeleo na kujumuishwa kwenye mpango na bajeti za Halmashauri;
 - (ix) Kujenga mazingira wezeshi na kutenga maeneo mahsusi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi kwa vikundi vya watu wenye ulemavu, vijana na wanawake;
 - (x) Kuainisha, kuchambua na kuwasilisha miradi yenye sifa za kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia kwenye mamlaka husika ili kupitiwa na kuidhishwa kwa mujibu wa Sheria ya Miradi ya Ubia Sura 103 iliyoifanywa marekebisho mwaka 2018 na Kanuni za mwaka 2015;
 - (xi) Kuhuisha na kuweka kwenye Tovuti za Halmashauri Mipango Mikakati ya Halmashauri, Mikakati ya Maendeleo ya Kiuchumi kulingana na vipaumbele vya maeneo husika na Wasifu wa Halmashauri kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, Malengo ya Maendeleo Endelevu, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Hati ya majukumu ya OR - TAMISEMI;
 - (xii) Kujumuisha kwenye mpango na bajeti za Halmashauri fedha zote kutoka kwa wadau wa maendeleo wa ndani na nje na vyanzo vingine;
 - (xiii) Kuomba idhini ya kuvusha matumizi ya fedha kwa mwaka unaofuata kabla ya tarehe 15 Juni 2020 na kutumia fedha hizo kabla ya tarehe 30 Septemba 2021 kwa mujibu wa Kifungu cha 29(3) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 na Kifungu cha 21(3) cha Kanuni za Bajeti;
 - (xiv) Kuzingatia Mwongozo wa OR-TAMISEMI wa utoaji wa vibali vya ujenzi na usimamizi wa ujenzi wa majengo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa uliotolewa Machi, 2018 na Mpango Mkakati wa Kuboresha Mazingira Wezeshi ya Biashara Nchini wa mwaka 2018;
 - (xv) Kutenga fedha kwa ajili ya usimamizi wa shughuli za Serikali na utoaji huduma katika ngazi ya Kijiji, Mtaa na vituo vya kutolea huduma;
 - (xvi) Kukuza fursa za ajira na uchumi wa maeneo husika kwa kuwajengea uwezo wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kuwapatia elimu ya biashara na ujasiriamali na kuwaunganisha na taasisi za fedha;
 - (xvii) Kuboresha shughuli za Huduma Ndogo ya Fedha kwa kuanzisha Kamati za Usimamizi, kuhuisha kanzidata ya vikundi vya fedha vya kijamii, kufanya usajili wa vikundi vya fedha vya kijamii na kuvijengea uwezo, kuvipatia mafunzo ya ujasiriamali, kuhamasisha urasimishaji wa watoa huduma ndogo za fedha, kufanya ufuatiliaji na tathmini na utoaji wa taarifa za vikundi vya fedha vya kijamii;

- (xviii) Kutenga fedha kwa ajili ya marejesho ya mikopo na michango ya wanachama kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa na kutenga fedha za kulipa mikopo kutoka taasisi za kifedha na Benki;
- (xix) Kuandaa mipango na makadirio ya Vituo vya Kutolea Huduma kama Shule, Vituo vya afya, Zahanati na hospitali na kujumuisha kwenye mpango na bajeti ya Halmashauri;
- (xx) Kuomba idhini ya Wizara ya Fedha na Mipango kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa kama ilivyoainishwa kwenye Waraka wa Hazina Na. 2 wa Mwaka 2019 kuhusu maelekezo ya kuomba na kuhamisha fedha za Washirika wa Maendeleo kwenda moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo (D – Fund) ikiwa ni pamoja na kuwasilisha orodha ya shughuli zitakazotekelezwa kwenye mradi;
- (xxi) Kutenga fedha za ujenzi, ukarabati na samani kwa ajili ya majengo ya utawala na nyumba za viongozi wa Halmashauri na Ofisi za Kata, Mitaa na Vijiji, kipaumbele ni kutekeleza miradi inayoendelea kabla ya kuanza miradi mipya; na
- (xxii) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya Mfuko wa Jimbo na TASAF kwa kila robo mwaka.

B. Maelekezo Mahsusi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Sekta za Afya, Elimu, Kilimo, Ardhi na Mazingira

- (i) Kuboresha huduma za afya na lishe katika ngazi ya jamii na vituo vya huduma za afya kwa kutenga fedha za uratibu, usimamizi na kujenga uwezo kuhusu masuala ya lishe ikiwa ni pamoja na kutenga shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano kwa ajili ya huduma za lishe;
- (ii) Kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango Kazi wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto na kuhakikisha Kamati za Watu wenye Ulemavu, Mabaraza ya Wazee na Kamati za Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto zinaanzishwa, zinahuishwa na kufanya kazi kwa mujibu ya Sheria, Miongozo na Taratibu;
- (iii) Kuboresha huduma za afya kwa kufanya yafuatayo: kujenga na kukarabati vituo vya kutolea huduma za afya na kuviwekea vifaa tiba na madawa, kuimarisha Bodi za hospitali za Wilaya, Timu ya uendeshaji wa shughuli za Afya ngazi ya Wilaya, kamati za vituo vya afya na zahanati na huduma za rufaa, kuboresha huduma za mama na mtoto ikiwemo huduma za chanjo, kudhibiti magonjwa yanayoambukizwa na yasiyoambukizwa, kuimarisha mfumo jumuishi wa usimamizi wa mashauri ya watoto walio katika mazingira hatarishi na kuhamasisha wananchi kujiunga na mfuko wa Afya ya Jamii na mifuko mingine inayotoa huduma za bima ya afya;
- (iv) Kuwatambua, kuwasajili na kuwaunganisha na huduma watoto walio katika

mazingira hatarishi wakiwemo watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani, wazee na watu wenye mahitaji maalum;

- (v) Kutekeleza mpango wa elimumsingi bila ada, kuhimiza michezo shuleni na katika ngazi ya Jamii pamoja na kuwasilisha Wizara za Fedha na Mipango kupitia OR - TAMISEMI takwimu za elimu zilizohuishwa zikijumuisha idadi ya wanafunzi, shule za awali, msingi, sekondari, waratibu elimu kata na shule za bweni ifikapo tarehe 30 Januari, 2020;
- (vi) Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule za msingi na sekondari kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya shule pamoja na kuwapatia nyenzo na vifaa wanafunzi wenye mahitaji maalum;
- (vii) Kuhakikisha wananchi wanapata huduma za ugani za kilimo, mifugo na uvuvi kwa urahisi, kudhibiti ubora wa pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kushirikiana na mamlaka za utafiti na udhibiti, ujenzi wa miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi pamoja na kuboresha ushirika na masoko ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi;
- (viii) Kuboresha shughuli za usimamizi wa mazingira kwa kuunda na kuimarisha kamati za mazingira katika ngazi za Halmashauri, Kata, Mtaa na Kijiji, kuhifadhi maeneo oevu na vyanzo vya maji, kutunza misitu na maeneo ya hifadhi, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuzingatia kanuni za udhibiti wa matumizi ya mifuko ya plastiki kwa mujibu wa zuio lililotolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais Mwaka 2019; na
- (ix) Kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, Sura 113 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji, Sura 114, kuweka mifumo ya mipango miji na matumizi bora ya ardhi kwa kuandaa mipango kabambe ya miji na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji ili kuwa na miji na vijiji vilivyopangika na kuweka alama za kudumu za mipaka ya kiutawala ya Kata, Vijiji, Mtaa na Vitongoji.

1.5. Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji

136. Ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti utazingatia Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 - 2020/21 pamoja na Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma.

1.5.1. Ufuatiliaji na Tathmini

137. Katika kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mpango na bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa:-

- (i) Kuandaa mpango kazi na mpango wa mahitaji ya fedha wa utekelezaji wa bajeti za Mafungu husika na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango;
- (ii) Kuweka mifumo thabiti ya ufuatiliaji na tathmini na kuhakikisha kuwa

malengo na viashiria vya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 - 2020/21 vinatafsiriwa vema katika mpango na bajeti;

- (iii) Kutoa mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini kwa watumishi wanaohusika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo;
- (iv) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na programu mbalimbali kwa kila robo mwaka;
- (v) Kuandaa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na programu mbalimbali na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango; na
- (vi) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya kisekta kwa pamoja.

1.5.2. Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji

138. Kwa mujibu wa Kifungu Na. 55(4) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni ya 29(5) ya Kanuni za Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa taarifa za utekelezaji za kila robo ya mwaka na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwasilisha nakala mango na tete za taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka mzima Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, OR-TAMISEMI (kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa) na Ofisi ya Msajili wa Hazina (kwa Mashirika na Taasisi za Umma).

139. Taarifa za Utekelezaji ziandaliwe kwa kuzingatia muundo ulioainishwa katika Sura ya Pili ya Sehemu ya Pili ya Mwongozo. Taarifa za utekelezaji za kila robo ya mwaka ziwasilishwe katika muda wa siku 30 baada ya kukamilika kwa robo ya mwaka husika. Vile vile, Taarifa za Utekelezaji za Mwaka ziwasilishwe kabla ya tarehe 15 Oktoba kila mwaka wa fedha.

SURA YA PILI

MUUNDO WA UWASILISHAJI NA UTOAJI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/21

2.1. Utangulizi

140. Sura hii inaainisha muundo na fomu pamoja na mambo muhimu ya kuzingatwa na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi nyingine za Umma wakati wa hatua za uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini pamoja na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mpango na bajeti.

141. Katika hatua hizo Maafisa Masuuli wanapaswa kuzingatia maelekezo yaliyopo kwenye nyaraka, mifumo na miongozo ya usimamizi wa: Mfumo wa Uandaaji na Usimamizi wa Bajeti (CBMS); Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango Mkakati wa Muda wa Kati na Bajeti (MTSPBM), Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 - 2020/21 (FYDP II-IS); Mwongozo wa Mfumo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Uandaaji wa Mpango na Utoaji Taarifa (PlanRep); Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (PIM-OM) na Mfumo wa Kuandaa Bajeti na Kutoa Taarifa za Utekelezaji katika Vituo vya Kutolea Huduma (FFARS).

2.2. Maandalizi ya Mpango na Bajeti

142. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa mpango na bajeti kwa kuzingatia Muundo wa Mapato na Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) kwa kujaza kikamilifu fomu Na. 1, 3, 4, 6, 7, 8, 9 na 10.

(a) Makadirio ya Mapato

143. Katika kuwasilisha makadirio ya mapato, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujaza kwa ufasaha fomu Na. 4 kwa kutumia mageresho sahihi.

(b) Makadirio ya Matumizi

144. Katika uwasilishaji wa makadirio ya matumizi, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuandaa makadirio ya matumizi mengineyo kwa kujaza fomu Na. 3A, 3B na 3C kwa kutumia vizio sahihi vya vipimo na gharama.

145. Maafisa Masuuli wanapaswa kuandaa makadirio ya mishahara kwa kujaza fomu Na. 8A-8F na fomu Na.9 kwa kuzingatia Ikama kama ilivyoidhinishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kipindi kinachoishia Juni 2021.

146. Katika kupanga makadirio ya matumizi ya maendeleo, Maafisa Masuuli wanapaswa kujaza kikamilifu Fomu Na. 6, 10A na 10C.

147. Kwa madhumuni ya kukusanya takwimu za ajira mpya, Maafisa Masuuli wanapaswa kujaza Fomu Na. 15A na kuziwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

2.3. Utekelezaji wa Bajeti

148. Mpango Kazi pamoja na Mpango wa Mahitaji ya Fedha ni nyenzo muhimu katika utekelezaji wa bajeti. Hivyo, baada ya bajeti kuidhinishwa na Bunge, Maafisa Masuuli wanapaswa kujaza kikamilifu kupitia mfumo wa CBMS fomu Na. 11A (R), 11A (D), 11B (R), 11B (D), 14B (R), 14B (D) na 14C na kuziwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango.

2.4. Taarifa za Utekelezaji

149. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuandaa na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango taarifa za utekelezaji za robo mwaka na mwaka kwa kuzingatia muundo uliotolewa. Fomu zinazopaswa kujazwa ni Na. 10B; 12A; 12B; 12C; 13A; 13B; na 13 (C1-C5). Aidha, Fomu Na. 15B inapaswa kujazwa na kuwasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

MUUNDO WA UWASILISHAJI WA MTEF 2020/21 - 2022/23

Maelezo ya Kisera kwa Ufupi

- i. Maelezo ya Waziri/Mkuu wa Mkoa/Meya au Mwenyekiti wa Halmashauri/Bodi
- ii. Maelezo ya Afisa Masuuli.

Sura ya 1: Uchambuzi wa Hali Iliyopo

- 1.1 Uchambuzi wa Wadau
- 1.2 Uchambuzi wa Uwezo, Udhaifu, Fursa na Changamoto
- 1.3 Masuala Muhimu ikijumuisha mawasilisho ya usimamizi wa vihatarishi.

Sura ya 2: Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti

2.1 Mapitio ya Utekelezaji - 2018/19

- 2.1.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2017/18
- 2.1.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi
- 2.1.3 Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi
- 2.1.4 Muhtasari wa Malengo yaliyopangwa yakilinganishwa na Malengo yaliyofikiwa

2.2 Mapitio ya Utekelezaji kwa Nusu Mwaka - 2019/20

- 2.2.1 Muhtasari wa Fedha zilizovuka mwaka kwa kila programu na maelezo ya matumizi 2018/19
- 2.2.2 Makadirio ya Mapato kwa Mwaka yakilinganishwa na Mapato Halisi
- 2.2.3 Makadirio ya Matumizi ya Mwaka yakilinganishwa na Matumizi Halisi
- 2.2.4 Muhtasari wa Malengo kwenye MTEF yakilinganishwa na Mafanikio yaliyopatikana

2.3 Changamoto zilizojitokeza 2019/20 na Mikakati ya baadaye

Sura ya 3: Makadirio ya MTEF (2020/21 - 2022/23)

- 3.1 Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti ya Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na.1)
- 3.2 Fomu ya MTEF inayoonesha Malengo Makuu, Malengo madogo na Shughuli zitakazofanyika - Kipande cha Pili (Fomu 3A)
- 3.3 Fomu ya Upangaji wa Gharama kwa Kila Shughuli (Fomu 3B)
- 3.4 Muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida (Fomu 3C)
- 3.5 Makadirio na Maoteo ya Mapato (Fomu Na.4)
- 3.6 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka na Miaka Miwili inayofuata (Fomu Na.6)
- 3.7 Muhtasari wa Matumizi ya Miradi ya Maendeleo (Fomu Na 6.1)
- 3.8 Mfumo wa Matokeo wa Kitaasisi (Fomu Na.7)
- 3.9 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa kila Fungu (Fomu 8A)
- 3.10 Muhtasari wa Makadirio ya Mishahara kwa Kifungu (Fomu 8B)
- 3.11 Kipengele Na.I - Muhtasari wa Wafanyakazi Walio kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara (Fomu 8C)
- 3.12 Kipengele Na.II - Muhtasari wa Wafanyakazi Wasio kwenye Orodha ya Malipo ya Mishahara (Fomu 8D)
- 3.13 Kipengele Na.III - Muhtasari wa Wafanyakazi Wanaotarajiwa Kuajiriwa (Fomu 8E)
- 3.14 Orodha ya Wafanyakazi Wanaotarajiwa Kustaafu (Fomu Na. 8F)
- 3.15 Jedwali la Mishahara kulingana na Ikama (Fomu Na.9)
- 3.16 Fomu ya Maelezo ya Mradi (Fomu 10A)
- 3.17 Taarifa ya Mradi ya Mpango wa Maendeleo na Tathmini ya Utendaji (Fomu 10B)
- 3.18 Muhtasari wa Makadirio ya Bajeti ya Miradi kwa mwaka unaofuata kwa Kila Fungu (Fomu 10C)

MUUNDO WA TAARIFA YA ROBO MWAKA

- I. Mada/Ukurasa wa Mbele wa Taarifa
- II. Yaliyomo
- III. Taarifa yenyewe

Utangulizi

- Maelezo kwa Ufupi ya Utekelezaji wa Hatua Muhimu/Shughuli za Kipaumbele:
- Sehemu hii ya taarifa ya robo mwaka inaelezea mafanikio ya utekelezaji wa hatua muhimu katika mchakato wa uandaaji wa mpango³.

Masuala mbalimbali na Vikwazo:

- Katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa hatua muhimu na shabaha, masuala mbalimbali na vikwazo vilivyojitokeza havina budi kubainishwa. Masuala hayo yanaweza kutokana na ucheleweshaji wa utekelezaji, kupungua kwa wigo au ubora wa kazi, vikwazo katika upatikanaji wa rasilimali, n.k. Ubainishaji wa masuala yanayopaswa kujumuishwa katika taarifa yatategemea jambo lenyewe. Hivyo, yanapaswa kupangwa kwa kipaumbele kulingana na namna yalivyoathiri kufikia malengo yaliyopangwa ndani ya kipindi husika.

Hatua za Kuchukua

Onyesha hatua za kuchukua katika kutatua masuala na vikwazo

- IV. **** Muhtasari wa Mabadiliko ya Bajeti na sababu zake (kwa Robo ya Pili pekee)**
- V. Viambatisho na Majedwali
 - Kiambatisho Na.1: Fomu 12A: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka ya Ufuatiliaji wa Malengo kwa Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati.
 - Kiambatisho Na. 2: Fomu 12B: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka ya Hatua Muhimu (Vipaumbele).
 - Kiambatisho Na.3: Fomu 13A: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka inayotoa Maelezo ya Hali ya Kifedha kwa Ufupi.
 - Kiambatisho Na. 4: Fomu 13B: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka kuhusu Taarifa ya Hali ya Kifedha kwa Kina.

Ufunguo: ** yajumuishwe katika Taarifa ya Mapitio ya Nusu Mwaka pekee

³ Katika kukusanya taarifa za utekelezaji wa hatua muhimu, Afisa anayehusika na uandaaji wa taarifa anapaswa kuwahoji watekelezaji ana kwa ana, badala ya kusambaza fomu husika ili zijazwe.

MUUNDO WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI YA MWAKA MZIMA

MADA/UKURASA WA MBELE

YALIYOMO

UTANGULIZI

1. Maelezo ya Waziri/Mkuu wa Mkoa/Meya/Mwenyekiti wa Halmashauri /Mwenyekiti wa Bodi
2. Maelezo ya Afisa Masuuli.
3. Muhtasari

TAARIFA YENYEWWE

1. **Sehemu ya Kwanza: Utangulizi.** Lazima ijumuishe yafuatayo:
 - Kifungu 1.1 (Utangulizi): Maelezo kwa ufupi kuhusu lengo la taarifa, mbinu na njia zilizotumika.
 - Kifungu 1.2 (Muundo): Inaelezea mpangilio na muundo wa taarifa.
2. **Sehemu ya Pili: Utekelezaji kwa Ujumla**
 - Kifungu 2.1 (Hatua iliyofikiwa): Hutoa dondoo muhimu za utekelezaji, kwa maneno na kwa muhtasari katika jedwali. Hufanya rejea katika viambatisho vilivyoelezewa kwa kina zaidi. Inapaswa kufanya rejea kwenye utekelezaji wa kufikia malengo na shabaha za SDG, FYDP II, au Ilani ya CCM 2015.
 - Kifungu 2.2 Hatua za kuboresha utoaji huduma (ubora, ufanisi, muda muafaka, au a- kuridhisha); jadili kuhusu mabadiliko yaliyotokea kwenye taasisi katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja. Kwa mfano, kama hati za kusafiria zinatolewa kwa haraka, kama gharama zimepunguzwa kutoka kwa mlipa kodi, n.k.
 - Kifungu 2.3 (Tathimini na Mapitio): Muhtasari wa matokeo ya tafiti zitakazotumika kuandaa taarifa ya Matokeo ya Miaka 3, na maendeleo kwa ujumla kulingana na tathimini.
 - Kifungu 2.4 Hatua Muhimu au Vipaumbele Vilivyotekelezwa: Mjadala kuhusu hatua muhimu ambazo zilipelekea kufikia lengo kwa ujumla au kufanikisha utekelezaji wa mpango.
 - Kifungu 2.5 (Vikwazo): Dondoo kuhusu matatizo au vikwazo na kubaini kwa umakini, shabaha ambazo hazikufikiwa na hatua zilizochukuliwa na menejimenti kushughulikia matatizo haya. Hii inaweza kuelezwa kwa kina katika Sehemu ya Tatu hapa chini.
3. **Sehemu ya Tatu: Mafanikio ya Shabaha za Mwaka.** Sura hii inapaswa kuwasilishwa kwa utaratibu wa Kifungu kwa Kifungu. Maelezo ya kina yatolewe kuhusu utekelezaji kwa kila shabaha na matokeo yaliyofikiwa. Sura hii pia inaweza kutoa maelezo ya kina juu ya shughuli muhimu (hususan zile ambazo hazijatekelezwa) na maelezo kwa ufupi juu ya takwimu za matumizi ya fedha yaliyokusudiwa kwa shabaha husika.
4. **Sehemu ya Nne: Hali ya Kifedha.** Sura hii ielezee kwa ujumla mwelekeo wa ukusanyaji mapato na matumizi ikilinganishwa na bajeti. Taarifa ya matumizi itokane na Mfumo wa Usimamizi wa Fedha (IFMS).
5. **Sehemu ya Tano: Mapitio ya Rasilimali Watu.** Muhtasari kuhusu rasilimali watu iliyopo, nafasi za kazi, na masuala mengine ya msingi ikiwa ni pamoja na uwiano kati ya stahili za mishahara na matumizi mengineyo.

VIAMBATISHO NA MAJEDWALI

- Kiambatisho Na.1: Fomu 12A: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka ya Ufuatiliaji wa Malengo kwa Mfumo wa Matumizi wa Muda wa Kati.
- Kiambatisho Na.2: Fomu 12B: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka ya Hatua Muhimu (Vipaumbele).
- Kiambatisho Na.3: Fomu 12C: Fomu ya Ufuatiliaji wa Viashilia vya Matokeo
- Kiambatisho Na.4: Fomu 13A: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka inayotoa Maelezo ya Hali ya Kifedha kwa Ufupi.
- Kiambatisho Na.5: Fomu 13B: Fomu ya Ujumla ya Robo Mwaka kuhusu Taarifa ya Hali ya Kifedha kwa Kina.

BUDGET PREPARATION FORMS

FORM 1: SUMMARY OF ANNUAL AND FORWARD BUDGET ESTIMATES FOR REVENUE, RECURRENT AND DEVELOPMENT EXPENDITURE
 ('000 SHILLINGS)

ECODE:

VOTE NAME:

Description		Actual	Approved Budget Estimates	Annual Budget Estimates	Forward Budget Estimates	Forward Budget Estimates
1		Yo-2	Yo-1	Yo	Yo+1	Yo+2
2		3	4	5	6	7
Revenue	Government Ceiling/ Grant					
	Loan					
	Own Source					
	Other Sources					
REVENUE						
Recurrent Expenditure	PE	PE for Vote proper				
		PE Subvention				
		PE Own source				
	Total PE					
	OC	OC for Vote Proper				
		OC Subvention				
		OC Own source				
	Total OC					
	Total Recurrent Expenditure					
	Development Expenditure	DEV Vote Proper	Govt. Funds			
Foreign Funds						
Own Source						

		Other Funds					
	DEV Subvention	Govt. Funds					
		Foreign Funds					
		Own Source					
		Other Funds					
Total Development Expenditure							
4. Remittance to Consolidated Fund							
TOTAL EXPENDITURE							

Note:

Revenue estimates = All available funds received from various sources

Total Revenue = Total Expenditure

Total Expenditure = Total Recurrent Expenditure + Total Development Expenditure

Total recurrent expenditure = Total PE + Total OC

Total PE = PE for vote proper + PE subvention

Total OC = OC for vote proper + OC subvention

Total Dev = Dev for vote Proper + Dev Subvention

Other Sources = Accrued interest, dividends, interest earned and other returns from investments

Other funds = Community contribution, PPP funds from private sector, etc.

Government Ceiling/Grant = Total ceilings or grants received from the Government

Own Source = Revenue collected that form part of institutions spending (MDAs, LGAs and Parastatals)

Loan = Borrowed funds that form part of institutions spending.

Other Sources = Funds received apart from loan, Own Source or Government grants

Vote Proper = Revenue collected and expenditure incurred within the same vote

Subvention = Government grant through vote proper

Y₀₋₂ = Two previous Years (2018/19)
Y₀₋₁ = Current Financial Year (2019/20)
Y₀ = Budget Year (2020/21)
Y₀₊₁ = Forward Budget (2021/22)
Y₀₊₂ = Forward Budget (2022/23)

FORM 3A: MTEF SHEET FOR OBJECTIVES, TARGETS AND ACTIVITY COSTING

VOTE CODE:

VOTE NAME

SUB-VOTE CODE:

SUB-VOTE NAME.....

Objective	Target	Target Type	Activity Code	Segment 2	Activity Description	Actual Y ₀₋₂	Approved Budget Estimates Y ₀₋₁	Annual Budget Estimates Y ₀	Forward Budget Estimates Y ₀₊₁	Forward Budget Estimates Y ₀₊₂
A										
	01									
		S								
			01	A01S01						
TOTAL										

Y₀₋₂ = Two previous Years (2018/19)
 Y₀₋₁ = Current Financial Year (2019/20)
 Y₀ = Budget Year (2020/21)
 Y₀₊₁ = Forward Budget (2021/22)
 Y₀₊₂ = Forward Budget (2022/23)

FORM 3B: ACTIVITY COSTING SHEET

VOTE CODE:
 SUB-VOTE CODE:
 OBJECTIVE NO:
 TARGET CODE:

VOTENAME
 SUB-VOTE NAME
 OBJECTIVE DESCRIPTION:
 TARGET DESCRIPTION:

Tick the appropriate (✓)
 FYDP II
 Other

Segment 2 Code	Segment 4 (GFS Code)	Required Inputs			Annual Budget Estimates <small>Y₀</small>		Forward Budget Estimates <small>Y₀₊₁</small>		Forward Budget Estimates <small>Y₀₊₂</small>	
		Segment 4 Description (GFS Code Description)	Unit of Measure	Unit cost of Inputs	No of Units	Estimates	No of Units	Estimates	No of Units	Estimates
1	2	3	4	5	6	7	8	9	10	11
TOTAL										

Notes

Column 1: Segment 2 includes objective, target, target type and activity;
 Column 7 equals column 5 x column 6
 Column 9 equals column 5 x column 8
 Column 11 equals column 5 x column 10
 Y₀ = Budget Year (2020/21)
 Y₀₊₁ = Forward Budget (2021/22)
 Y₀₊₂ = Forward Budget (2022/23)

FORM 3C: RECURRENT EXPENDITURE SUMMARY OF DRAFT ESTIMATES

VOTE CODE:
 SUB-VOTE CODE:

VOTE NAME
 SUB-VOTE NAME

Segment 4 (GFS Code)	Segment 4 Description (GFS Code Description)	Actual Budget Y ₀₋₂	Approved Budget Estimates Y ₀₋₁	Annual Budget Estimates Y ₀	Forward Budget Estimates Y ₀₊₁	Forward Budget Estimates Y ₀₊₂
(1)	(2)	(3)	(4)	(5)	(6)	(7)
TOTAL						

Notes

Columns 5, 6 and 7 is a Summary of Form No. 3(b) Activity Costing Sheet

- Y₀₋₂ = Two previous Years (2018/19)
- Y₀₋₁ = Current Financial Year (2019/20)
- Y₀ = Budget Year (2020/2021)
- Y₀₊₁ = Forward Budget (2021/22)
- Y₀₊₂ = Forward Budget (2022/23)

FORM 4: REVENUE ESTIMATES AND PROJECTIONS

VOTE CODE:
 SUB-VOTE CODE:

VOTE NAME
 SUB-VOTE NAME

Segment 4 (GFS Code)	Description	Actual Collection Y ₀₋₂	Approved Estimates Y ₀₋₁	Draft Estimates Y ₀	Forward Budget Y ₀₊₁	Forward Budget Y ₀₊₂	Remarks
(1)	(2)	(3)	(4)	(5)	(6)	(7)	
14220122	Tender Document						
	Total of Sub -Vote						
	TOTAL OF VOTE						

Notes:

- Y₀₋₂ = Two previous Years (2018/19)
- Y₀₋₁ = Current Financial Year (2019/20)
- Y₀ = Budget Year (2020/21)
- Y₀₊₁ = Forward Budget (2021/22)
- Y₀₊₂ = Forward Budget (2022/23)
- Remarks = Reason for significant decrease or increase of revenue

FORM 6: DEVELOPMENT EXPENDITURE DETAILS OF ANNUAL AND FORWARD BUDGET

VOTE CODE:
 SUB-VOTE CODE:
 PROJECT CODE:
 OBJECTIVE NO:
 TARGET CODE:

VOTE NAME
 SUB-VOTE NAME
 PROJECT NAME:
 OBJECTIVE DESCRIPTION:
 TARGET DESCRIPTION:.....

Tick the appropriate (✓)
 FYDP II
 Other

(Seg. 2) Performance Budget Codes	Activities Description	Segment 4 (GFS Code)	Segment 4 (GFS Code Description	Annual Budget Estimates Y ₀						Forward Budget Estimates Y ₀₊₁			Forward Budget Estimates Y ₀₊₂		
				Local	Foreign	L/G	D	Donor	Total	Local	Foreign	Total	Local	Foreign	Total
(1)	(2)	(3)	(4)	(5)	(6)	(7)	(8)	(9)	(10)	(11)	(12)	(13)	(14)	(15)	(16)
	Total of Target														
	Total of Project														
	TOTAL OF SUB-VOTE														

Notes

Total Target is Sum of all activities under a Target
 Total Project is Sum of all targets under a Project
 Total Sub-Vote is Sum of all Projects under the Sub-Vote
 Total = Local fund + Foreign fund
 L/G = Loan/Grant
 D = (Direct to project)

Y ₀ = Budget Year (2020/21) Y ₀₊₁ = Forward Budget (2021/22) Y ₀₊₂ = Forward Budget (2022/23)
--

FORM 6.1: SUMMARY OF DEVELOPMENT PROJECTS EXPENDITURE ESTIMATES

Project code	Project Name	Annual Budget Estimates Y ₀				Forward Budget Estimates Y ₀₊₁			Forward Budget Estimates Y ₀₊₂			
		Local		Foreign		Total	Local	Foreign	Total	Local	Foreign	Total
		Government	Own Source	L/G	D							
(1)	(2)	(3)		(4)	(5)	(6)	(7)	(8)	(9)	(10)	(11)	(12)
	Total of Sub Vote											
	Total of Vote											

Notes

L/G = Loan/Grant

D = (Direct to project)

Y₀ = Budget Year (2020/21)

